# KUCHUNGUZA DHIMA ZA NYIMBO ZA SINGO KATIKA KIJIJI CHA UZINI ZANZIBAR

**MWAKA MWINYI WAZIRI**

**TASNIFU NDOGO ILIYOWASILISHWA, KUWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGIRII YA UZAMILI YA KISWAHILI (FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2016**

## UTHIBITISHO

Aliyesaini hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa: "**Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Singo Katika Kijiji cha Uzini Zanzibar"**, ninapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili ya Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

……………..………………………….

Profesa, Dkt. Sk. Mwl. T.Y.S.M Sengo

(Msimamizi)

………………………….……………

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile iwe yote ama sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali za utafiti, kijisomea au kufanya marejeleo ya kitaaluma bila ya kibali cha mwandishi wa tasnifu hii au cha Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, Mwaka Mwinyi Waziri ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyengine yoyote.

…………………………………………….

Saini

…………………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Ninapenda kuitabaruki kazi hii kwa wazazi wangu, mume wangu, walimu wangu na watoto wangu.

## SHUKURANI

Kazi hii ya utafiti ni matokeo ya mchango wa ushirikiano mkubwa sana baina yangu na watu kadhaa wakiwemo walimu wangu. Wafuatao wanastahiki shukrani za kipekee.

Kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai, uzima, nguvu na fahamu katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M Sengo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua hadi utafiti huu kumalizika. Msaada wake hauwezi kukisiwa kwa thamani yoyote ila nasema ahsante sana Profesa Sengo. Mwenyezi Mungu ambariki na amjaalie afya njema na maisha marefu yenye manufaa duniani na akhera. Aaamin, Aaamin, Aaamin.

Tatu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wangu wengine wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa msaada wao mkubwa walionipatia katika kipindi chote cha masomo yangu. Walimu hao ni pamoja na Profesa Emmnuel Mbogo, Dk. Zelda, Dk. Omar Adam, Dk. Grace, na Dk. Omar Moh’d kwa kunipatia miongozo mema katika utafiti wangu huu.

Nne, ninapenda kumshukuru sana mume wangu bwana Mohammed Kassim Hassan pamoja na watoto wangu. Kassim Mohammed Kassim, Zainab Mohammed Kassim na Fatma Mohammed Kassim kwa kuwa na ustahamilivu kwa shida zote zilizowakabili katika kipindi chote cha harakati za kimasomo.

## IKISIRI

Utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kuchunguza dhima za nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini Zanzibar. Katika kutimiza lengo hilo data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji pamoja na mbinu ya ushuhudiaji katika maeneo ya Uzini Mshomarini, Mitakawani, Tunduni, Mpapa na Mgeni Haji, ambapo sherehe za singo zilifanyika. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu za mkabala wa kimaelezo. Nadharia za Fasihi Ina Kwao, Dhima na Kazi pamoja na nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika zilitumika katika kubainisha dhima hizo kwa jamii ya watu wa Uzini, ambazo zilisaidia kubaini utamaduni wa Mswahili kupitia kijiji hicho. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba nyimbo za singo ambazo ni sehemu ya fasihi simulizi, zina siri kubwa na ni mwalimu tosha wa kumpatia mwanamwari taaluma ifaayo kukabiliana na maisha yake ya ndoa. Kwa vile utafiti huu ulichunguza dhima za nyimbo za singo ukimlenga hasa mtoto mwanamke, utafiti umetoa hitimishi la moja kwa moja kwamba, jamii ya Waswahili hasa ya Kizanzibari, bado inaendeleza utamaduni wa kuwasinga wanawari kwa kutumia nyimbo ambazo zinatoa mafundisho yaliyo mema kwa lengo la kuwaandaa na maisha yao katika ndoa. Vilevile, utafiti umependekeza tafiti zaidi zifanyike kwa vijana wa jinsia ya kiume na kuangalia mafanikio kwa wanandoa waliofanyiwa mila na dasturi hii. Utafiti huu una manufaa kwa jamii hususani kwa vijana ambao wanajiandaa kukabiliana na maisha mapya ya ndoa, kwa vile uchunguzi uliofanywa umebaini kuwa, nyimbo za singo zilitoa mchango mkubwa wa mafunzo kwao. Zinalenga kuwaandaa katika kuyakabili maisha yao kiuhalisia zaidi. Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti alikabiliwa na matatizo kama vile ya uhaba wa

wataalamu wa fani hiyo ya nyimbo za singo, maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yaliaathiri sana upatikanaji wa taarifa za utafiti huu kwa vile wazee ambao ni mahiri kwa kutongoa nyimbo hizo walionekana kupoteza nafasi zao kwa kuwa na ushiriki mdogo katika shughuli hizo na kupelekea kupotea kwa nyimbo hizo katika vichwa vyao na kusababisha upotevu wa nyimbo za asili za singo. Aidhani, utafiti huu ulikabiliwa na tatizo la uhaba wa marejeleo yanayokwenda sawia na mada ya utafiti huu.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**
**HAKIMILIKI** ........ **iii**
**TAMKO** ........ **iv**
**TABARUKU** ........ **v**
**SHUKURANI** ........ **vi**
**IKISIRI** ........ **vii**
**ORODHA YA VIAMBATANISHO** ........ **xii**
**SURA YA KWANZA** ........ **1**
**UTANGULIZI KWA UJUMLA** ........ **1**
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Usuli wa Mada ........ 1
1.2.1 Singo ........ 1
1.2.2 Jando na Unyago ........ 2
1.2.2.1 Jando ........ 2
1.2.2.2 Unyago ........ 3
1.3 Tatizo la Utafiti ........ 6
1.4 Lengo Kuu La Utafiti ........ 7
1.4.1 Madhumuni Mahasusi ........ 7
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 8
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 8
1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 8
1.8 Vikwazo vya Utafiti ........ 9
1.9 Utatuzi wa Vikwazo ........ 9

**SURAYA PILI** ........................................................................................ **11**

**UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA** .......... **11**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 11

2.2 Maana ya Nyimbo ........................................................................................ 11

2.2.1 Aina za Nyimbo ........................................................................................ 13

2.2.2 Dhima za Nyimbo ........................................................................................ 14

2.3 Mkabala Wa Kinadharia ........................................................................................ 16

2.3.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika ........................................................................................ 16

2.2.2 Nadharia ya Fasihi Ina Kwao ........................................................................................ 16

2.3.3 Nadharia ya Dhima na Kazi ........................................................................................ 17

**SURA YA TATU** ........................................................................................ **19**

**MBINU ZA UTAFITI** ........................................................................................ **19**

3.1 Utangulizi ........................................................................................ 19

3.2 Muundo wa Utafiti ........................................................................................ 19

3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................ 19

3.4 Walengwa wa Utafiti ........................................................................................ 20

3.5 Uteuzi wa Watafitiwa ........................................................................................ 20

3.6 Vyanzo vya Data za Utafiti ........................................................................................ 20

3.6.1 Data za Msingi ........................................................................................ 21

3.6.2 Data za Upili ........................................................................................ 21

3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........................................................................................ 21

3.7.1 Usaili ........................................................................................ 22

3.7.2 Ushuhudiaji ........................................................................................ 22

3.7.3 Hojaji ........................................................................................ 23

3.8 Maadili ya Utafiti ........................................................................................ 23

**SURA YA NNE.................................................................................................... 24**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA................................................ 24**

4.1 Utangulizi ........................................................................................................ 24

4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data ............................................................. 24

**SURA YA TANO ................................................................................................ 47**

**HITIMISHI NA MAPENDEKEZO ..................................................................... 47**

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 47

5.2 Muhtasari.......................................................................................................... 47

5.3 Hitimishi........................................................................................................... 48

5.4 Mapendekezo ................................................................................................... 49

**MAREJELEO ....................................................................................................... 50**

**VIAMBATANISHI ............................................................................................... 53**

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanishi 1: Hojaji La Utafiti Kwa Watafitiwa ................................................ 53

Kiambatanishi 2: Nyimbo Zinazoimbwa Katika Sherehe za Singo.......................... 57

Kiambatanishi 3: Ramani ya Kisiwa cha Unguja Ikionesha Maeneo ya Utafiti....... 68

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI KWA UJUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imejumuisha usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, matatizo ya utafiti pamoja na njia za utatuzi wa matatizo hayo.

## 1.2 Usuli wa Mada

### 1.2.1 Singo

Katika jamii nyingi za Kiafrika watu hufanya sherehe za matukio tafauti yanayotokea siku hadi siku. Matukio hayo ni pamoja na sherehe za singo, sherehe ya jando na unyago, sherehe ya harusi, sherehe za mwakakogwa, sherehe za kuzawa, sherehe za kuhitimu masomo na hata sherehe za kuapishwa viongozi.

Singo ni miongoni mwa sherehe muhimu sana inayofanywa ndani ya jamii ya Waswahili, hasa katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa kawaida sherehe hizo hufanyiwa binti siku moja kabla ya kufunga ndoa. Mara nyingi hufanyika wakati wa usiku (magharibi na kuendelea) ambapo jamii hulenga kutoa mafundisho yaliyo mema kwa binti.

Sherehe za singo kuwapo kwake kunatokana na urithi kutoka kwa wazee. Kina bibi tokea uhai wao, walifanya sherehe hizo kwa lengo la kutoa mafunzo yahusuyo ndoa kwa mabinti zao. Wakati wa kufanyika sherehe hiyo, somo wa binti (Kungwi), huandaa zana zake ambazo huzitumia katika kufanikisha singo. Zana zenyewe ni

kama vile mafuta ya nazi, karafuu iliyosagwa na liwa. Kila moja, kati ya zana hizo, hutumika kwa lengo lake maalumu.

(a) Mafuta ya nazi, hupakwa binti katika mwili wake wote, isipokuwa katika sehemu zake za siri tu. Mafuta hayo, yana sifa ya kuufanya mwili uwe mwororo.

(b) Karafuu na liwa, hutumika kwa pamoja, kumsugulia binti katika mwili wake wote. Karafuu na liwa, huwa na kazi ya kuutia mwili nguvu na kuziondosha takataka zilizobaki mwilini kwa muda mrefu (Maryam: 2016).

Somo wa bi harusi akishirikiana na wenzake humsinga mwari kwa kumsugua mwili wake wote. Wakati shughuli hii ikiendelea, nyimbo huimbwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa binti mhusika kuhusu maisha yake ya ndoa anayotaka kuyaingia. Kimsingi, kupitia sherehe hiyo ya singo, jamii hupata fursa nzuri ya kujifunza, kuburudika, kuonyeka, na kuhadharishwa juu ya ubora wa kuyatekeleza mambo mema na kuyawacha yale yote yanayokatazwa.

### 1.2.2 Jando na Unyago

#### 1.2.2.1 Jando

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Fasaha (2010), jando ni pahali wanapowekwa watoto wa kiume wanapotahiriwa. Jando ni zaidi ya tendo la kumtahiri mtoto wa kiume. Ni chuo Kikuu cha mafunzo ya maisha.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004), inafafanua dhanna ya jando kama ni chuo Kikuu cha watoto wanaume, wanapotahiriwa na kufundishwa mambo ya kiutu uzima. Fasili hii inatufundisha kuwa, jamii nyingi duniani zinapowatayarisha watoto wao wa kiume kuingia ukubwani, huwapa mafunzo yanayoweza kuwaongoza katika

kipindi chote cha utu uzima wao, kwa kutahiriwa na kufunzwa yaliyo mema. Katika kipindi hicho, watoto wa kiume hukaribishwa ukubwani.

Haji na wenzake (1981), wanatubainishia dhanna ya jando kwa kusema:

> Kutokana na mila za jamii watu huwa wanatambulishwa rasmi mabadiliko hayo. Mfano ngoma za jadi, jando na unyago zimo katika jamii za Kiafrika ambapo jando kwa kawaida ilikuwa kwa wale wavulana ambao wameshakuwa wakubwa, kiasi ambacho wanataka waelewe wajibati zao, kuhusu namna ya kuishi katika jamii kwa marika hayo waliyofikia.

Vijana huingizwa jandoni wakiwa na umri kuanzia miaka saba na kuendelea. Wavulana baada ya kutahiriwa wakisubiri kuvuka, walipatiwa mafunzo juu ya maadili bora kuwaheshimu wakubwa, kuwa shupavu, uwajibikaji, jinsi ya kuishi vizuri na mke, namna za kulinda familia, ukoo na kabila kwa jumla. Yalikuwa mafunzo ya kuwaingiza vijana katika utu uzima.

**1.2.2.2 Unyago**

Ni Chuo Kikuu cha vijana wa kike mahali maalumu, ili kufundishwa maelekezo ya mila na dasturi za kabila lao. Tendo hilo kwa kawaida hufanyiwa wasichana ambao wamekwisha vunja ungo. Ni tukio maalumu kwa wasichana fulani waliokwishatoka katika kundi la watoto na sasa wamo katika kundi la watu wazima.

Msichana alichezwa unyago kuanzia umri wa miaka saba na kuendelea, na kwa kawaida msichana akishachezwa unyago huwa tayari kwa maisha ya ndoa. Wasichana walifundishwa jinsi ya kutunza nyumba, jinsi ya kutunza watoto, jinsi ya kufanya mapenzi na kujistarehesha na kuwastarehesha waume zao. Zanzibar ni

visiwa, watu wake wa asili tofauti yakiwemo makabila ya Wazaramo, Wamakonde, Wamakua, Wakurya. Yote hayo ni makabila maarufu kwa shughuli hizi.

Jando na unyago ni shughuli zilizoimarika. Wanajamii wa nyakati zilizopita waliuona unyago kama chuo Kikuu chao cha kutoa mafunzo kwa mabinti, na jando kwa vijana wa kiume. Mzee Suleiman Abdalla Suleiman alisema:

> Mimi ninavyofahamu, wari hufundishwa namna ya kuishi vizuri na waume, pamoja na kuwahudumia, kuwatunza waume, watoto na familia kwa jumla. Na kijana wa kiume barobaro, hufundishwa jinsi ya kuishi vizuri na mke. Hivyo, wanajamii wa nyakati hizo walithamini na kutukuza harakati hizo kwa kuwa ilikuwa ni darasa tosha kwa watoto wao katika kujenga jamii yao kwa kufuata mila na dasturi zao.

Kwa jumla sherehe za singo, jando na unyago ni sherehe ambazo zina mfanano kwa walengwa walio sawa. Lengo kuu la sherehe hizo ni kuwaandaa vijana na mabinti kukabiliana na maisha ya utu uzima (maisha ya ndoa), kila mmoja kwa nafasi yake.

Kama jamii nyengine za Kiafrika, Waswahili nao walitumia nyimbo katika sherehe zao za kijamii. Mwanajamii yoyote kazaliwa na kupewa jina la kitoto, kapitishwa jandoni au unyagoni, harusini hadi kifoni. Nyimbo huimbwa katika sherehe zinazohusu mambo ya kila siku, kazi, mapumziko na michezo. Hayo ndiyo yaliyomsukuma mtafiti kuchunguza nini hasa kilichomo ndani ya nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo.

Wazanzibari kama Waswahili wengine wana sanaa zao, silka, dasturi na mila zao, ambazo wamerithi kutoka kwa bibi na babu zao, mila ambazo, kama Waswahili

wenyewe wanavyosema, “Mrithi hurithi chake na kutoka kwa mstahiki wake”. Urithi wa utamaduni wa Mzanzibari hauko katika ngoma tu bali ni bahari pana yenye kina kirefu cha maji. Urithi wa mema ya utamaduni ndiyo dira na msingi imara ambao utaendelea kuimarishwa na kunufaisha vizazi na vizazi vya uswahilini. Ardhi ya Kiswahili ni moja ya tanzu za kurithiwa na Waswahili. Asiye Mswahili asitiye tope mirathi ya watoto halali waliozawa Uswahilini.

Kwa mujibu wa mchoro wa ramani ya urithi wa utamaduni wa Zanzibar wa Idara ya Maendeleo ya Utamaduni wa Zanzibar (2010), Uongozi wa serikali umeazimia:

(i) Utamaduni hujieleza ambapo lugha ya Kiswahili ndicho chombo kikuu cha mawasiliano ya urithi huo.

(ii) Sanaa, mila, imani, dasturi, ndiyo muhimili wa jamii imara wa kusimamisha utamaduni fulani, ambapo mtafiti kwa nafasi yake alipata fursa ya kuiamsha jamii, kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wa Mzanzibari uliyomo katika nyimbo za singo.

(iii) Kuuendeleza umilikifu wa urithi wa utamaduni kwa kusimamisha haki ya kurithisha kwa vizazi vijavyo.

Kimsingi, hii ni fursa adhimu ya kuwatanabahisha wale wanaodhani kuwa ngoma tu ndio utamaduni na kuyawacha mambo mengine ya msingi katika urithi wa utamaduni huo. Utamaduni ni mfumo mzima wa maisha ya jamii.

(a) Mila, hujumuisha mambo ya malezi, tiba za asili, mazindiko, harusi, kifo, jando, unyago na nyimbo zikiwamo za singo.

(b) Dasturi, ni kawaida za jamii, kama vile, maamkizi, kutembeleana, kusaidiana, kuheshimiana, adabu njema na maadili mema.

(c) Itikadi, hujenga mambo ya kiroho, imani za jadi, mielekeo ya kisiasa na ushirikiano wa kijamii.

(d) Sanaa, inahusisha lugha katika utenda kazi wake, kwenye fasihi na lughawiya.

(e) Kazi, inahusisha kazi za asili zilizokuwa zikifanywa katika jamii, mfano ukulima, uvuvi, uwashi, ufuaji vyuma pamoja na uundaji wa majahazi, mitepe, madau na mashua, ukwezi, biashara na ufugaji, zote ni miongoni mwa kazi za Waswahili,

Kimsingi, utamaduni una dhima kubwa sana katika jamii, kwa sababu unaelezea na kusimamia namna ya kuyaendesha maisha kugusa katika kila jambo linalomhusu mwanadamu na jamii kwa jumla pamoja na kuuenzi na kuudumisha muhimili huo wa kimaisha.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Nyimbo za singo zimekuwa zikifanya kazi ya kusawiri maisha halisi ya jamii ya Waswahili. Kutokana na mchango mkubwa wa nyimbo hizo katika kukuza na kujenga maadili mema kwa jamii ndipo mtafiti akaona ni vyema kuingia kiundani kutimiza wajibu wake wa kuchunguza dhima za nyimbo hizo, kwani singo ni tukio kubwa lililojificha kwa tiba za mwili na ualimu wa maisha ya ndoa.

Watafiti wengi wamefanya utafiti wao kuhusu nyimbo Mfano, Mbarouk (1983) amefanya utafiti kuhusu nyimbo za michezo ya watoto. Ameir (1998) alifanya utafiti kuangalia mafunzo yaliyomo katika nyimbo za watoto. Khamis (1980) alifanya utafiti kuhusu ujumbe unaopatikana katika nyimbo za taarab. Katika watafiti wote hao hayuko aliyefanya utafiti juu ya nyimbo za singo na hasa kuishughulikia hiyo

siri iliyomo katika tukio hilo la kumsinga biharusi kwa madawa na nyimbo. Mnani ndani ya siri hiyo? Hili ndilo tatizo hasa lilimfanya mtafiti kujiingiza katika taaluma hiyo.

Mara tu baada ya jamii kuingia katika hadazi za maendeleo ya sayansi na teknolojia, jamii nyingi zilibadili mwelekeo wake na kutoa mafunzo kwa wanandoa kwa kutumia nyimbo zisizoimbwa katika sherehe za singo. Inaonekana wazi jamii imepoteza mwelekeo wake kwa vile nyimbo hizo sasa zimo kutoweka. Hali hiyo itaifanya jamii kupoteza urithi wa mila na dasturi zake. Khasara za kutoweka kwa taasisi za jadi kama vile unyago na jando Visiwani, inaonekana kwenye ndoa na talaka zisizo mashiko. Majuto ni mjukuu'. Leo hii mihimili ya mafunzo yahusuyo ndoa imepoteza nafasi zake, tukisema tuzirudishe tena dasturi hizo masomo, makungwi na manyakanga wako wapi?

## 1.4 Lengo Kuu La Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima za nyimbo za singo zinazoimbwa katika sherehe ya kumfunza mwanamwari kwa lengo la kumuandaa na maisha ya ndoa.

### 1.4.1 Madhumuni Mahasusi

Utafiti huu una madhumuni mahasusi yafuatayo:

**1.4.1 .1** Kubainisha nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za singo.

**1.4.1. 2** Kuchambua dhima za nyimbo za singo kwa wanandoa watarajiwa katika kijiji cha Uzini.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na jumla ya maswali mawili ambayo yanasaidia kukamilisha lengo kuu na madhumuni mahasusi ya utafiti huu. Maswali hayo ni:

(a) Je, ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika sherehe za singo?

(b) Je, ni dhima gani zinazopatikana katika nyimbo za singo kwa wanandoa watarajiwa?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatafaa kuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wataalamu ambao ni walimu, wahadhiri pamoja na maprofesa katika taaluma ya fasihi, wataweza kutumia utafiti huu katika kuandika vitabu na makala ambazo zitachukua nafasi ya kutunza mila na dasturi za jamii.

Kwa kupitia utafiti huu watafiti wajao wataona umuhimu wa kutumia nadharia za Fasihi Ina Kwao, Dhima na Kazi, katika kuhakiki masuala tofauti ya kazi za fasihi. Utafiti huu ni kishawishi cha kuimarisha sera ya Utamaduni mwema wa Mswahili, Zanzibar, kwa kuzitathimini nyimbo maarufu zinazoimbwa katika sherehe ya singo.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza dhima za nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini kilichopo Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. Uteuzi wa eneo hilo umefanywa kwa sababu ndiko ambako mtafiti amezaliwa na kulikuwa pia na wepesi wa lugha na upatikanaji wa data.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti huu umekumbana na vikwazo vifuatavyo:

### (a) Uhaba wa wataalamu

Wataalamu wa fani ni wachache, ilimwia vigumu mtafiti kuweza kuzinasa taarifa zihusuzo utafiti huu. Watafitiwa walio wengi walikataa kumpatia mtafiti taarifa za utafiti kwa kutoa sababu za kuhifadhi siri za singo.

### (b) Uhaba wa marejeleo

Aidhani, utafiti huu ulikumbana na tatizo la uhaba wa marejeleo ambayo yanakwenda sambamba na mada ya uchunguzi. Kwa kutumia nadharia ya sanaajadiiya, masikani kwa watafitiwa, ndiko kama maktaba au chanzo kikuu, cha upatikanaji wa taarifa za utafiti, (Sengo: 1985).

### (c) Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Kikwazo chengine ni uvulivuli wa fahamu kuhusu sayansi na teknolojia, ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa za utafiti huu. Kina bibi ambao wamekuwa na umahiri mkubwa wa kutongoa nyimbo hizo za singo wameonekana kupoteza nafasi zao, hivyo kusababisha upotevu wa taasisi ya nyimbo za singo. Kikwazo hiki cha kuiga wageni (kwa jina la usasa) kitaigharimu sana Zanzibar na Afrika kwa jumla.

## 1.9 Utatuzi wa Vikwazo

Utatuzi wa vikwazo ni jambo muhimu sana ambalo husaidia kukamilika kwa utafiti. Katika kuhakikisha kwamba utafiti huu unakamilika kwa wakati, mtafiti alilazimika kusafiri kwenda kwenye vyuo vikuu vyengine kama vile, Dodoma, UDSM , kwa

lengo la kuwafuata wataalamu mfano Profesa Emmanuel Mbogo (OUT), Dk Athumani Ponera (Dodoma), Profesa T.S.Y.M. Sengo (Taasisini kwake AERA-DSM ), kuwahoji.

Kwa upande wa tatizo la maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambayo yanaonekana kuwanyang'anya mabibi nafasi zao za kutongoa nyimbo za singo, nimejaribu kuwahamasisha wazee hao kuwa tayari kushirikiana na vijana kuendeleza suala hilo muhimu kwa lengo la kufufuwa, kuimarisha, na kurithisha utamaduni kwa vizazi vijavyo.

Kwa upande wa marejeleo, mtafiti alitumia marejeleo machache yaliyopo kwa lengo la kukidhi matakwa ya utafiti.

# SURAYA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mada ya dhima za nyimbo za singo, kwa taarifa alizonazo mtafiti, bado haijafanyiwa utafiti. Ingawa watafiti wengi waliotangulia walijaribu kuandika kuhusu nyimbo kwa miktadha tafauti.

Msokile (1981), Nkwera (1993), Njogu na wenzake (1999), Sengo (1995), Gibbe (1980) na Robbert (2004) walitoa mchango mkubwa wa taarifa kwa mtafiti lakini tafiti zao hazikuingia katika kuchunguza dhima za nyimbo za singo.

## 2.2 Maana ya Nyimbo

Hamad na wenzake (1972), wameeleza kuwa nyimbo ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Nyimbo inaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi. Nyimbo huweza kuimbwa na kuchezwa kwa kutumia muziki au kipekee.

Msokile (1981) anafasili nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Wasanii huimba nyimbo baada ya kupata mguso fulani ndani ya jamii. Sanaa ya nyimbo inatafautiana na sanaa ya mazungumzo kwa sababu ya matumizi ya lugha pamoja na vionjo maalumu vya kishairi vinavyoleta mvuto kwa jamii.

Balisidya (1987), anaeleza kuwa nyimbo ni tungo za kishauri, zenye kutumia mahadhi ya melodi, mapigo na muwala. Nyimbo huimbwa na watu ambao hujaribu

kuelezea maisha. TUKI (1987) inafafanua kuwa ushairi hujumuisha nyimbo. Nyimbo ni moja mwa tanzu muhimu katika ushairi. Inatoa maana ya nyimbo kuwa ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988), inaeleza maana ya nyimbo kuwa ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, meledia, mapigo na muwala. Nkwera (1993), ameeleza kuwa nyimbo huambatana na uimbaji, anasisitiza kuwa nyimbo ni lazima iundwe na mambo mawili ambayo ni maneno yanayoimbwa na yawe yanamfunza mwanadamu katika mazingira yake.

Njogu na wenzake (1999), wameeleza kuwa nyimbo zinatokana na ushairi ambao ndio utanzu wa Fasihi ulio mkongwe, nyimbo ambazo zilianza na hisia za matukio yaliyowakuta watu katika mazingira yao ya raha na furaha, ugumu wa kujituma ama machungu na ushujaa. Wanafafanua kwa kusema kuwa, katika jamii za kilimwengu wimbo ulianza wakati mwanadamu alipobuni lugha, jambo ambalo lilimtoa katika hali ya uhayawani na kumfanya awe kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mwanadamu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango katika kuyakabili na kuyabadilisha mazingira hayo.

Mtafiti ameibuka na dhanna kuwa nyimbo ni tungo zenye mapigo maalumu ya sauti, ambayo huimbwa au hutongolewa na wanadamu kwa lengo la kufikisha ujumbe maalumu.Wasanii hao hutongoa nyimbo zao hizo kwa lengo la kuwapatia wanandoa watarajiwa maelekezo yaliyo mema kwa maisha yao ya ndoa.

### 2.2.1 Aina za Nyimbo

Finnegan (1970), anasema nyimbo zinaweza kutofautiana katika muundo, mtindo, maudhui, au dhima. Lakini zina kitu kimoja ambacho huzifanya zote zifanane, nacho ni usimulizi. Kutokana na tofauti hizo Finnegan ameziweka nyimbo katika makundi mbalimbali. Miongoni mwao ni nyimbo za kisiasa, nyimbo za watoto, nyimbo za kazi, kama vile kilimo, uvuvi, ukwezi, ulinzi na uwindaji. Nyimbo hizo zinaelezea mambo yanayaojitokeza katika jamii kama vile kufunza, kuelimisha, kubururdisha na kuliwaza.

TAKILUKI (1981), imezungumzia kuhusu nyimbo za maombolezo. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar inasema kuwa, jamii nyingi za Kiafrika nyimbo hutumika wakati wa msiba, nyimbo ambazo wakati mwingine huwa kama kasida na huimbwa katika nyakati tafauti. Kwa mfano hapa Zanzibar, nyimbo hizi huimbwa wakati wa kupamba maiti, kubeba jeneza na kuelekea makaburini, baada ya mazishi na wakati wa kumkumbuka marehemu. Katika Afrika, nyimbo hizi huimbwa katika nchi ya Nigeria na Ghana.

Mbarouk (1983), ameandika kitabu cha nyimbo za michezo ya watoto. Katika kitabu hiki Mbarouk anasema, kila jamii ya watu huwa na michezo yao ya jadi ambayo huchezwa na watoto wa jamii ile. Michezo hii mara nyingi huambatana na nyimbo. Katika kisiwa cha Pemba kwa mfano, iko michezo mingi ya watoto ambayo hutofautiana kutoka sehemu moja na nyengine, jambo ambalo ni muhimu katika michezo hii ni nyimbo ambazo ndizo zinazochukuwa nafasi ya uzuri wa michezo hiyo.

Mulokozi (2013) amegusia aina za nyimbo za Kiafrika, na kuziweka katika makundi kama vile, nyimbo za kidini, nyimbo za kazi, nyimbo za vita, nyimbo za Taifa, nyimbo za kuwindia, nyimbo za watoto, nyimbo za jando na unyago na nyimbo za harusi. Nyimbo zote hizo, zinasimulia na kuelezea mambo yanayotokea katika jamii zikiwa na lengo la kufunza, kuelimisha na kukosoa.

Kwa mujibu wa maelezo ya watalamu hao mtafiti anaibuka na aina za nyimbo ikiwemo nyimbo za singo, ambayo ndiyo mada ya utafiti huu, ikichunguza dhima ya nyimbo hizo. Ni miongoni mwa makundi ya nyimbo zinazoimbwa katika jamii hususani jamii ya Kizanzibari, ambazo hulenga kutoa mafunzo ya kiadilifu na maelekezo kwa wanandoa watarajiwa.

### 2.2.2 Dhima za Nyimbo

Lucas (1975), amaezungumzia kuhusu nyimbo za msanja na jando ambazo ni katika utamaduni wa mwafrika. Mfano Zanzibar nyimbo hizi huimbwa sana katika maeneo ya Kusini mwa visiwa hivi ambazo hulenga kutoa mafunzo, malezi na maadili mema yanayowasaidia wanajamii kujua namna ya kuishi kulingana na matumizi ya nyimbo hizi. Nkwera (1978), kwa upande wake anafafanua nyimbo kuwa ni kipengele muhimu cha ushairi ambacho hubeba mafundisho ya hekima na malezi ya busara. Maelezo ya Mtaalamu huyu yalimsaidia sana mtafiti kuweza kubaini nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo katika kijiji cha Uzini.

Msokile (1981) anafafanua dhamira za nyimbo kuwa ni lazima zilingane na hadithi, zikubaliane na jamii katika kupokea ujumbe. Gibbe (1980) nae kwa upande wake

anafafanua kuwa nyimbo hutumika katika kuwaelimisha wanandoa kuwa na maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, hekima na kuwa na adabu nzuri. Ameir (1998), amegundua kuwa nyimbo za watoto zina tafsri kubwa kiutamaduni, kimaisha na kimalezi. Kupitia utafiti huu, mtafiti amepata fursa ya kugundua siri iliyomo ndani ya nyimbo za singo kwa jamii ya watu wa Uzini.

Seif (2011), anasema unyago humuandaa mwanamke (msichana) kukabiliana na utu uzima, hii ni pamoja na ndoa, miiko ya mila na mafunzo ya maisha kwa ujumla. Unyago ni chuo muhimu sana kwa jamii. Huko unyagoni mabinti walielekezwa kujitunza na kuwa waangalifu ili kuepuka kupata uja uzito bila ya mpangilio (kabla ya kuolewa). Nyimbo zilitumika sana kuhakikisha kuwa elimu inawaingia mabinti hao. Pia miiko ya jamii ilielekezwa kwa njia ya nyimbo. Kwa ujumla unyagoni binti hufundwa mambo mengi sana ya maisha na kwa yule aliyeweza kuyashika kikamilifu na kuyatumia basi alionekana kuwa ni binti mwenye heshima kubwa na aghlabu alipata mchumba wa kumuoa mapema sana katika jamii hiyo.

Mtafiti ameibuka na wazo la jumla kuwa, nyimbo zote zinazoimbwa katika jamii huwa na makusudio yake. Mfano, nyimbo za kubembelezea watoto huimbwa kwa lengo la kuwaliwaza watoto na kuwafariji wazazi. Nyimbo za jando na unyago huimbwa kwa lengo la kuwaadaa wanawari pamoja na vijana kwa maisha ya kiutu uzima.

Makungwi, masomo, wanandoa pamoja na wasanii wa nyimbo za singo, huimba nyimbo hizo kwa lengo la kuwaadaa wanandoa watarajiwa kuweza kuyakabili maisha yao ya ndoa.

## 2.3 Mkabala Wa Kinadharia

Sengo (2009), anaifasili dhanna ya nadharia kuwa ni muongozo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsusi kwa kutoa maoni, mwelekeo au falsafa juu ya matumizi ya taratibu za utafiti.

### 2.3.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika

Nadharia hii ilitiwa mwega na Sengo (1970). Nadharia hii ina misingi katika jamii za Kiafrika. Imejengwa katika mazingira halisi ya jamii. Nadharia hii ilikuwa dira ya kumuongoza mtafiti katika kuzielewa nyimbo zilizoimbwa katika sherehe za singo katika mazingira yake hali pamija na dhima zake kwa lengo la kumpatia mwanamwari mafundisho yaliyo mema kwa ajili ya maisha ya ndoa yake.

### 2.2.2 Nadharia ya Fasihi Ina Kwao

Muasisi wa nadharia hii ni Sengo (2009). Katika nadharia hii anasisitiza kuwa ili kuieleza fasihi ya jamii fulani, mtu ni lazima kulijua eneo husika, mila, dasturi, silka, kaida na mema ya utamaduni wa jamii hiyo.

> "Fasihi ya Kiswahili, kwao ni Uswahilini, Pwani Mwambao wa Afrika Mashariki, ambako kuna jadi zao, katika viambo vyao, makaazi yao, vijiji vyao na miji yao"

Fasihi simulizi ina sifa zake maalumu zinazofanana duniani kote, lakini inapaswa kutambuliwa kuwa kila jamii ina fasihi yake ya kipekee. Kulingana na mtazamo wa nadharia hii, jamii huasisi utamaduni na utamaduni humtambulisha mwanajamii. Utamaduni ni bahari yenye sanaa na sanaa huunda fasihi. Fasihi inajumuisha nyimbo ambazo ndani yake zimesheheni mafunzo toshelevu kwa jamii husika.

Nadharia hii ilimsaidia sana mtafiti kubainisha nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo pamoja na dhima zake kwa jamii ya wanandoa watarajiwa katika kijiji cha Uzini. Nyimbo za singo ni sehemu ya Fasihi simulizi ambazo zinachukuwa nafasi ya mila na desturi ya jamii ya watu wa Uzini. Akina bibi walipokuwa wakijiandaa kuozesha watoto wao, waliitayarishia sherehe hiyo maalumu kwa wanandoa watarajiwa. Wakati wa kuwasinga wari, walikuwa imara kwa kazi ya kutoa miongozo kwa mabinti kwa lengo la kufanikisha ndoa zao.

### 2.3.3 Nadharia ya Dhima na Kazi

Nadharia ya dhima na kazi imeasisiwa na Sengo (2009). Nadharia hii huzichambua kazi za fasihi kwa kuangalia dhima zilizomo ndani yake. Kazi yoyote ya fasihi hutumiwa kwa lengo maalumu. Mfano, nyimbo kama kitanzu cha fasihi Simulizi hutumiwa kwa lengo maalumu kama vile kuburudisha, kuonya, kukosoa, kuelimisha. Hivyo, mawazo ya Sengo kupitia nadharia ya Dhima na Kazi yamemuelekeza mtafiti kugundua dhima za nyimbo za singo, kwa vile sherehe hiyo ni moja ya matukio muhimu sana katika utamaduni wa Zanzibar, sherehe ambayo inatongoa siri za ndani ya maisha ya ndoa.

Ili kuchunguza dhima za nyimbo za singo ni lazima tuchunguze matumizi ya nyimbo zenyewe nyimbo ambazo haziimbwi burebure tu, bali huimbwa kwa lengo maalumu la kutoa mafunzo yanayomuongoza mwari katika kuyakabili mazingira yake ya ndoa. Dhima kuu ya nyimbo za singo ni kuwalekeza wanandoa namna ya kuyaingia na kuyaishi maisha mapya na khalisi ya ndoa.

Mtafiti ameamua kutumia nadharia hizo kwa sababu ya mapungufu ya nadharia moja kwa nyengine. Mfano, nadharia ya Dhima na Kazi haiwezi kutosheleza matakwa ya

utafiti huu. Imeweza kumpatia mtafiti muongozo kuhusiana na dhima ya nyimbo za singo tu na si vyenginevyo, na hapo ndipo mtafiti alipooa ni vyema kujihusisha na nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika, ambayo ilimuwezesha mtafiti kukamilisha malengo yake ya utafiti kwa kuweza kuangalia mambo yote yahusuyo utafiti wake kama vile kubaini nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo pamoja na dhima zake kwa jamii ya wanandoa watarajiwa.

Kwa muktadha huo tunaweza kusema kwamba, nadharia zote hizo tulizozieleza ni zenye kufaa katika utafiti huu, kwa sababu zimeweza kumsaidia mtafiti kuchambuza nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo pamoja na dhima zake kwa jamii lengwa.

(a) Nyimbo za singo huimbwa katika mazingira halisi ya kumsugua (kumsafisha) mwanamwari kuepukana na yale yote ambayo yataweza kuiharibu ndoa yake. Mfano, wakati singo linapoendelea, kungwi na wenzake wanapomsugua mwari katika mwili wake kwa kutumia liwa na karafuu, hali hiyo husawiri upya atakaoupata mwanamwari wa kiroho na kimwili, kwa kuwacha na kufuata yote atakayoelekezwa kupitia nyimbo hizo (Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika).

(b) Nyimbo za singo huimbwa kwa lengo maalimu. Lengo kuu la nyimbo hizo, ni kumuandaa mwanamwari kwa maisha yake ya ndoa, kwa kumpatia mafunzo na maadili yafaayo (Nadharia ya Dhima na Kazi).

(c) Nyimbo za singo huimbwa katika jamii maalumu, hususani Zanzibar kikiwemo kijiji cha Uzini (Nadharia ya Fasihi Ina Kwao).

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea mbinu na njia za utafiti ambazo mtafiti alizitumia. Vipengele ambavyo vimebainishwa, ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, uteuzi wa watafitiwa na mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti au uchunguzi makini, ulitumia muundo wa kimaelezo katika kukusanya na kuchambua data. Utafiti wa kimaelezo kwa mujibu wa Cohen na wenzake (2007) ni utafiti ambao hupanga na kutoa sababu pamoja na kuziwasilisha data kama zilivyotolewa na walengwa wa utafiti.

Katika utafiti huu tumeteua na kuzichambua nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo. Nyimbo hizo zikiwa ni kitanzu cha fasihi simulizi zinalengo kutoa mafunzo, maadili na maelekezo yaliyo mema kwa wanawari wanaoandaliwa kuyaingia maisha yao ya ndoa.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Unguja, katika Mkoa wa Kusini Unguja maeneo ya Uzini Mshomarini, Mitakawani, Tunduni, Mgenihaji na Mpapa. Sababu za kuteua maeneo hayo ni kwamba wanajamii hao wanatumia sana sherehe za singo kwa lengo la kuwaandaa mabinti zao wakati wakiwa tayari kufunga ndoa.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Cooper (1989) na Varis (1990) wanafasili kundi lengwa ni wanachama wote au hata mtu mmoja au wawakilishi ambao mtafiti amekusudia kuwahusisha katika utafiti wake. Hivyo katika utafiti huu walengwa wa utafiti ni wasanii wa nyimbo za singo, wataalamu wa taaluma ya fasihi, wanandoa wanaoshiriki mara kwa mara katika sherehe za singo, masomo na makungwi ambao kwa kawaida huwa na wajibu mkubwa wa kumfunza mwari kabla ya kufunga ndoa.

### 3.5 Uteuzi wa Watafitiwa

TUKI (1981) anaeleza kuwa uteuzi ni uchaguzi makini wa kitu miongoni mwa vitu. Uteuzi wa watafitiwa aghlabu huwa ni wachache wanaochaguliwa kuwakilisha vitu vinavyofanyiwa uchunguzi ili kupata taarifa za uchunguzi huo. Katika utafiti huu tulitumia uteuzi kusudio katika kuwapata watafitiwa.

Kwa mujibu wa Kothari (2009), uzuri wa utafiti ni wa mtafiti kuchagua watoa taarifa wanaofaa katika utafiti wake. Uteuzi kusudio humsaidia mtafiti kupata watoa taarifa anaowataka. Utafiti huu ulihusisha watafitiwa arubaini (40), wakiwamo wasanii wa nyimbo za singo, wataalamu wa Fasihi, wanandoa wanaoshiriki mara kwa mara kwenye sherehe za singo, makungwi na masomo. Watafitiwa wote hao walichaguliwa kwa kuzingatia kigezo cha nafasi zao kwa vile wao, ndiwo waliokidhi sifa za utafiti huu.

### 3.6 Vyanzo vya Data za Utafiti

Adam na wenzake (2007) wanasema data za utafiti zinaweza kukusanywa kwa njia ya maelezo au takwimu. . Kuna vyanzo vikuu viwili vya data, data za msingi, na data

za upili. Hivi ndivyo vyanzo vikuu vya data ambazo zilikusanywa na kutumika katika utafiti huu.

### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data zilizokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kutoka masikanini. Kothari (2004) kwa mujibu wake, hizi ndizo data ambazo hukusanywa kutoka kwa wahojiwa, ambazo ndizo data halisi. Data hizo mtafiti huzipata uso kwa uso kutoka kwa watoa taarifa wake wa masikanini. Kupitia hali hii mtafiti alifanikiwa kuzinasa nyimbo kadhaa zinazoimbwa katika sherehe ya singo pamoja na dhima zake kwa jamii ya wanandoa watarajiwa.

### 3.6.2 Data za Upili

Adam na wenzake (2007) wanaelezea data za upili kwamba, hukusanywa kutoka katika vyanzo kama vile vitabu, majarida, na magazeti. Data hizo huwa zimechapishwa au huwa zinapatikana Maktabani na Mitandaoni. Mtafiti katika utafiti huu alikusanya data katika maktaba kwa kuangalia tafiti za wataalamu mbalimbali kama vile Msokile (1981), Nkwera (1983), Mulokozi (2003), Gibbe (1980), Seif (2011). Tafiti ambazo zinahusiana na nyimbo katika nyanja tofauti zilimuongoza mtafiti katika kutafiti nyimbo za singo pamoja na dhima zake kwa jamii ya wannandoa watarajiwa.

## 3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004) ukusanyaji wa data ni zoezi la awali ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia, ili kumfikisha kwenye

madhumuni yake ya utafiti. Hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanikiwa kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data.

### 3.7.1 Usaili

Ni mbinu ambayo taarifa hukusanywa kwa njia ya kuuliza maswali ya ana kwa ana au kwa simu ya mkononi. Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu ya usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo huhusisha kuuliza maswali kwa njia ya mdomo. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kukusanyia data za utafiti wake, mbinu ambayo ilimpa fursa mtafiti kuweza kuelewa nyimbo kadhaa ambazo huimbwa katika sherehe za singo. Mtafiti aliamua kutumia njia hiyo kwa sababu ilimrahisishia upatikanaji wa taarifa kwa watafitiwa. Aidha, njia hii ilimrahisishia mtafiti kuwahoji watafitiwa wengi kwa muda mfupi. Wasanii wa nyimbo za singo, wanandoa wanaoshiriki mara kwa mara katika sherehe ya singo, makungwi na masomo dio waliofanyiwa usaili na kutoa majibu yaliyosaidia sana katika kufanikisha utafiti huu.

### 3.7.2 Ushuhudiaji

Ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti hukusanya data akiwa katika uasili wake. Kwa mujibu wa Kothari (2004*)* ushuhudiaji ni mbinu ambayo taarifa hukusanywa na mtafiti mwenyewe kwa kushuhudia tabia za watafitiwa, awasikilize, awafahamu kwani mbinu hii ni ya umakinifu wa mtafiti, kukubalika kuwa yu mmoja miongoni mwa washiriki, ili aweze kupata data za utafiti wake.

Katika utafiti huu, mtafiti alishuhudia mwenyewe jinsi wasanii, makungwi, masomo na wanandoa walivyoshiriki katika kuimba nyimbo za kumsinga mwari. Ushiriki wa watafitiwa hawa ulimsaidia mtafiti kuchambua nyimbo zinazoimbwa katika shughuli

ya kumsinga mwari pamoja na mafunzo na maelekezo yaliyo mema kwa wanandoa hao.

### 3.7.3 Hojaji

Kothari (2004) anafafanua dhanna ya hojaji kuwa ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti huandaa maswali yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mfano, ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika sherehe ya singo? Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti na ilimsaidia kuzielewa nyimbo za singo na dhima zake kwa wanandoa watarajiwa. Kwa kutumia mbinu hiyo, mtafiti aliwapa hojaji, walimu na wakufunzi wa shule za sekondari ya juu nao waliyajaza na kuyarejesha. Taarifa za wahojiwa hao zilimsaidia mtafiti katika kufanya uchanganuzi wa utafiti wake.

## 3.8 Maadili ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti hakuwa na budi kuelezea maadili ya utafiti. Kwa mujibu wa Seture (2010) mkabala wa maadili ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti alipaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alizitambua haki zote na kuzifanyia kazi, ambapo aliwaelezea watafitiwa kuwa palipotokea tatizo, mtafiti alichukua dhamana ya kuwajibika.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika sehemu mbili. Uwasilishaji na uchambuzi wa nyimbo za singo na dhima zilizomo ndani ya nyimbo hizo ikiwa ni pamoja na kumuadilisha na kumfunda mwari kuhusiana na maisha ya ndoa.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Mtafiti alikwenda masikanini kukusanya data ambazo katika maeneo aliyoyachagua. Watu aliowateua walikuwa wasanii wa nyimbo za singo, wataalamu wa fasihi, wanandoa walioshiriki katika sherehe za singo, masomo na makungwi. Mtafiti alifanikiwa kuwahoji washiriki wote hao, nao wameweza kumpatia mtafiti data alizokusudia. Kwa mujibu wa watafitiwa hao, nyimbo kumi na nane za singo zilikusanywa, kumi na tatu kati ya hizo zilifanyiwa uchambuzi.

**1. MUME**

Ukitaka mume akae, kutandika kuna maanae

Ukitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi

Ukitaka mume adumu, kutandika kuna maalumu

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Msanii ametumia mandhari ya chumbani ambako ndiko kunakopatikana ukamilifu wa ndoa yenyewe. Msanii ametumia taswira ya kitanda kilichotandikwa kwa lengo la kutaka kuufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa wanandoa watarajiwa.

Wimbo huu umeundwa katika mfumo wa mafumbo ambapo lugha iliyotumika imeficha baadhi ya mambo na kumuachia msikilizaji aweze kutafakari na kuibua maana iliyokusudiwa kwa wanandoa watarajiwa. Kitanda ndicho kipumbazi na kipumzishi cha uchovu wa wanandoa. Kikitandikwa vizuri, kitanda husema, hucheka, huvutia, na huwatuliza wanandoa wakajiona wameshafika peponi. Familia huanza na kitanda. Mke, mama, mlezi wa aila, kiongozi wa familia huyafanikisha yote hayo kwa kukitandika vizuri kitanda.

**DHIMA**

Wimbo huu hulenga kumfunza mwanamwari mambo ya kuifanya ndoa yake idumu. Wimbo huu unaweka wazi mbinu ambazo humlaghai mume na kumteka akili ili aweze kuishi kwa amani, raha mustarehe ndani ya ndoa.

Kwanza, wimbo unalenga kumfahamisha mwanadoa mtarajiwa umuhimu wa kutandika kitanda chake, ambacho atakilalia yeye na mume wake, ndipo hapo anapoambiwa kuwa "ukitaka mume akae, kutandika kuna maanae" Maana yenyewe ni huko kupumbazika, kupumzika na kuburudika.

Dhima ya wimbo huu, kutandika kitanda kuna maana gani kwa wanandoa? Kimsingi jibu la suala hilo ni zito na ni muhimu kwa wanandoa watarajiwa kuweza kulitafakari, kwa makini sana katika maisha yao ya ndoa.

Kwa mujibu wa mtafitiwa bibi Maryamu Moh'd Ali wa Mitakawani, kutandika kitanda maana yake ni kujitayarisha kwa kumpokea mume kwa kumtimizia haki yake ya msingi katika ndoa. Maandalizi yatakayooneshwa na mke kitandani, ni dalili tosha itakayomdhihirishia mume juu ya mapokezi hayo, na hapo ndipo mume naye

kwa upande wake atakapojiweka tayari kwa hilo. Kila mmoja ni nguo na pumbazi kwa mwenziwe.

Pili, wimbo huu unatoa mafunzo kwa mwanamwari juu ya mitindo ambayo itamvutia mume katika tendo la ndoa chumbani mwake, mitindo ambayo huwa na maana maalumu. Bibi Maryamu Ali, aliifafanua mitindo hiyo, ambayo inapotandikwa kitandani hutoa ishara maalumu kwa mume. Mfano, mtindo wa ndege wawili ambao huelekezana midomo. Shuka hizi zinapotandikwa mume moja kwa moja huelewa kwamba, kwa siku hiyo, hakuna jengine isipokuwa ni mazungumzo na mipango ya kimaisha tu. Vilevile, kuna mtindo wa kuwekwa kikuba katikati ya kitanda, mtindo huo unaashiria kuwa ni siku ya kupeana chakula (kufanya tendo la ndoa) baina yao.

Tatu, wimbo huu pia unalenga kumfunda mwanamwari kumuenzi, kumlea, kumtunza, kumnyenyekea, na kumbembeleza mume wake. Mambo hayo ndiyo yatakayomfanya mume adanganyike, aliwazike, na aridhike na maisha, baina yake na mke wake. Msanii alisema, mume ni mtu anayependa sana kuenziwa, kutukuzwa, kubembelezwa, kunyenyekewa. Alimfananisha mume sawa na mtoto mdogo kwa huduma anazohitaji kupatiwa kutoka kwa mke wake wa ndoa. Hivyo wimbo unabeba dhima ya kumpatia mwanamwari fundisho hilo kwamba, akitaka mume akae kutandika kuna maanae, akitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi na akitaka mume adumu, kutandika kuna maalumu.

Mafundisho ya wimbo huu kwa wanandoa watarajiwa yanaonekana kuwa na mafungammano makubwa na nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika. Kwa wakati huu wa maendeleo makubwa ya sayansi na teknologia, kiuhalisia tunawaona wanandoa kuwa

na mafungamano makubwa ya kutayarisha vitanda vyao kwa kuvitandika kwa kutumia shuka zenye mapambo ya kila aina na mitindo tofauti. Wanandoa wa nyakati hizi ni wenye kufuatilia na kuyatekeleza yale mambo yote ambayo yanajaribu kuwaweka karibu na waume zao, kama vile kupamba nyumba zao, kutandika vitanda kwa mitindo tofauti, kutunza usafi wa nyumba zao, yote yakiwa na lengo la kumlaghai na kumteka mume.

**2. KUNGWI**

Kungwi mwambie mwario

Asiwache ufunguo

Akiwacha ufunguo

Watafungua wenziwe,

Na kama hakufyagia

Watafyagia wenziwe,

Na kama hakutandika

Watatandika wenziwe,

Na kama hakufukiza

Watafukiza wenziwe,

(Bi Bahati Rajab: Uzini Kibombani: 2016)

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Msanii katika wimbo huu ametumia neno ufunguo, neno ambalo linajenga dhanna pana katika nyumba ya mwanamke lenye maana ya hifadhi. Ufunguo wa maisha ya ndoa unamilikiwa na mwanamke, yeye ndiye mficha siri za ndani ya nyumba yake baina yake na mume wake. Yeye ndiye mlezi wa mume wake na aila yake akiwa

mzembe na kuiwacha hazina hiyo wazi, mke huyo atakuwa ameshindwa na ndoa yake.

**DHIMA**

Wimbo huu unatoa mafundisho yafuatayo kwa mwanamwari:

Kwanza, awe makini katika ndoa yake. Msanii anasema,

Kungwi mwambie mwario
Asiwache ufunguo
Akiwacha ufunguo
Watafungua wenziwe"

Wanawari hawatakiwi kuwa na dharau na uzembe katika masuala ya kumtunza mume na ndoa kwa jumla. Wanawari wakiyafanya hayo wanawake wengine watachukuwa nafasi ya kubadili ndoa zao.

Pili, mke awe ni msafi wa nyumba yake, msanii anasema:-

Na kama hakufyagia
Watafyagia wenziwe
Na kama hakufukiza
Watafukiza wenziwe"

Waswahili wanasema **"**mwanamke usafi". Suala la kutunza usafi wa nyumba kwa wanandoa ni suala lililopewa kipaumbele na wasanii wa nyimbo za singo.

Masuala ya kufyagia na kutandika kitanda, yanaiweka nyumba katika hali ya usafi na unadhifu. Bibi Bahati Rajab, alisema, mwanamke aliye katika ndoa, anapaswa kuitunza nyumba yake kwa kuisafisha vizuri na kutandika kitanda vizuri sana. Chumba daima kiwe kisafi na nadhifu.

Tatu, wimbo huu unalenga kumfunza mwari juu ya mila, dasturi na utamaduni wa Mswahili wa Kizanzibari. Ni suala la kufukiza udi. Udi ni uturi unaotengenezwa kwa kutumia sukari, manukato, pamoja na vijiti fulani fulani. Mke anatakiwa afukize chumba chake kila siku kwa kuuchoma udi ambapo harufu nzuri itaenea katika chumba hicho, hali ambayo humvuta mume kulifikia lengo la ndoa. Ni kishawishi kinachoamsha hisia za kimapenzi kwa mwanamume dhidi ya mkewe. Hivyo kupitia wimbo huo, msanii anawasisitiza wanandoa watarajiwa wafikapo katika ndoa zao wawe makini na suala hilo kwani vitu kama hivyo ndivyo vinavyojenga mapenzi na raghba katika ndoa.

Maelezo haya yote yanakwenda sambamba na maelezo yaliyotolewa na Msokile (1981). Alisema kuwa dhamira za nyimbo ni muhimu zilingane na hadithi, kwa maana ya kwamba ujumbe unaopelekwa kwa jamii ukubaliane na jamii yenyewe. Kwa mintarafu hii, ni wazi kwamba dhima za wimbo huu ni zenye kukubalika kwa jamii ya wanandoa watarajiwa, wakiwa na lengo la kudumisha ndoa zao.

Aidha, Soyinka (1975), anasema kuwa “mwanamke ni pambo la mwanamume”. Hivyo mwanamke wakati wote anatakiwa kuwa msafi kwa mume wake na jamii iliyomzunguka. Maelezo ya mtaalamu huyu yanakwenda sawia na dhima ya wimbo huu.

Kwa upande wa nadharia, nadaharia ya Uhalisia wa Kiafrika ni muafaka sana kwa uchambuzi wa dhima hizi. Katika hali halisi mwanamke anatakiwa awe safi wakati wote na katika mazingira yake yote.Vilevile, anapaswa kuwa makini katika kuichunga ndoa yake, hana budi kuyatekeleza yale yote ambayo yataijenga na kuipendezesha ndoa yake muda wote.

**3. MSUMARI WA KIZUNGU**

"Msumari wa kizungu, haulali yeka

Hata bafuni, haulali yeka

Hata sebuleni, haulali yeka

Hata jikoni, haulali yeka"

**MAELEZO KUHUSU**

Neno "msumari wa kizungu" limetumika likimuwakilisha mume rijali. **"**Haulali yeka*"*, lina maana ya kwamba, mume kawaida yake halali pweke kitandani. Anapohitaji kukidhi matamanio yake, basi hachagui sehemu maalumu, ni popote mradi pana faragha. Suala la kubakwa kwa mke na mume halipo. Mkataba wa mke kuolewa ni kuwa tayari kwa hilo wakati wowote na popote penye sitara kwa tendo hilo.

**DHIMA**

Dhima kubwa ni kuheshimu haki ya kisheria kwa mke kumtimizia mume wake. Mafundisho ya Dini ya Kiisilamu yanawafundisha wanawake kuwatimizia waume zao haki hiyo. Inasemekana bi Fatma binti Rasuli aliweka magodoro katika kila

sehemu iliyokuwa ni sitara ndani ya nyumba yake kwa lengo la kumtimizia mume wake haki hiyo ya msingi. Mwanamwari anafundishwa awe tayari kumtekelezea mumewe haki yake ya msingi pahala popote na wakati wowote ila anapokuwa na udhuru wa safari zake.

Bi Asha Ramadhani wa Mpapa alisema, mwanamke mara tu baada ya kuingia katika ndoa yake anatakiwa kulipa kipaumbele suala la kutimiza haki ya msingi kwa mume wake. Suala hilo ndilo linaloitimiza ndoa na bila ya kutendeka basi hakuna ndoa. Pindipo watakuwa washupavu juu ya kutimiza haki hiyo wakinyanyapaa, watajenga uchukivu kwa waume zao na hata kwa Muumba wao.

Mtaalamu Nkwera (1978) anashadidia dhima ya wimbo huu kwa kusema kwamba, nyimbo ni kipengele muhimu sana cha ushairi ambacho hubeba mafundisho ya hekima na malezi ya busara katika kipindi cha maisha ya malezi ya mwanadamu. Katika kipindi hiki maisha ya mwanadamu huamabatana na mafunzo ndani yake. Haya tunaweza kuyathibitisha ndani ya wimbo ambapo unatoa fundisho kubwa kwa wanandoa watarajiwa la kuwatimizia waume haki zao za msingi katika ndoa.

Kwa upande wa nadharia, nadaharia ya Dhima na Kazi inaonekana kuchukua nafasi kubwa katika ufafanuzi wa wimbo huu. Katika mazingira ya kawaida lengo kuu la ndoa ni mwanamke kumtimizia mume haki yake ya msingi. Hili ndio hasa linalompeleka kwa mume, mwanamke ni kipumbazi cha mwanamume kwa njia ya halali.

Aidha, nadahria ya Uhalisia wa Kiafrika pia imechuka nafasi katika uchambuzi wa dhima za wimbo huu. Mfano, katika hali halisi mke huozwa mume kwa lengo la

kumstarehesha mume wake, nako ni huko kumtimizia haki hiyo ya msingi katika ndoa. Panaposhindikana utekelezaji wa suala hilo, migogioro baina ya wanandoa hawa yaweza kutokea jambo ambalo linaweza kuhatarisha ndoa.

**4. MWENYE HARUSI**

Mwenye harusi yu wapi, aniazime kitabu

Mwari wake amekuwa, kuolewa ni wajibu

Wala asione haya, hili jambo la thawabu

Sote tumeyakutia, kaanza bibi na babu

Mume ukamwite bwana, usende kumwita babu.

Mume ukampe raha, usende kumpa tabu."

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo huu huimbwa wakati mwanamwari ameshawekwa utangani tayari kwa kusingwa. Utanga ni sehemu maalumu ambayo huwekwa mwari wakati anapofanyiwa singo. Somo, kungwi na wapambe wengine humtaka mama harusi kusogea karibu kumfunda mtoto wao.

**DHIMA**

Wimbo huu una dhima kubwa zifuatazo kwa wanandoa:

(a) Suala la ndoa ni suala la wajibu

Msanii anatoa fundisho kwa wanandoa watarajiwa kwamba, suala la ndoa si suala la kihiari bali ni suala la lazima kwa kila atakaefikia umri wa kufanya hivyo. Kwa mujibu wa mafundisho ya Dini ya Kiislamu, ndoa ni wajibu kwa kila aliyefikia

baleghe, mwanamke na mwanamme. Kulitekeleza suala hili ni ukamilifu wa ibada. Humtoa mja nuksani na kumjengea heshima kwa jamii iliyomzunguka. Msanii anasema:

"Mwari wako amekuwa, kuolewa ni wajibu"

Hivyo, tunamuona msanii hakuwa nyuma katika kutoa muongozo mwema juu ya suala la kisheria kwa wanadamu katika maisha yao ya kila siku.

(b) Suala la ndoa ni suala la thawabu

Msanii anatoa mafundisho hilo wanandoa watarajiwa. Mtafitiwa, Bi Aviwa Idd wa Tunduni, aliyahusisha maneno ya Bwana Mtume Muhammad (SAW) kwamba, mja atakapofungamana na tendo la ndoa kihalali, malipo yake ni thawabu nyingi tokea mwanzo hadi mwisho na kukataa kutimiza jambo hilo kwa mume wa ndoa ni laana kubwa zitokazo kwa Muumba. Mke ni wa mume na mume ni wa mke.

Mafundisho hayo yanaendelea kutujuvya kwamba maji yatakayodondoka kutokana na josho la wawili hao (mke na mume wanapojitoharisha kutokana na tendo walilolifanya) huuwa majini sabiini waovu wanaoishi chooni na ni fadhila kubwa kwa wanandoa. Msanii anawahimiza wanandoa watarajiwa wawe tayari kuyatimiza yaliyo wajibu katika ndoa zao kwa lengo la kupata radhi za waume na za Mola wao kwa jumla.

(c) Suala la kuheshimiana katika ndoa

Suala la heshima katika ndoa baina ya mke na mume limepewa kipaumbele na wasanii wa nyimbo za singo. Msanii anawapatia wanandoa watarajiwa mafunzo yahusuyo heshima. Mume ni kiumbe duni kinachopenda kutukuzwa, kunyenyekewa,

kuheshimiwa, kubembelezwa na kuenziwa. Mke naye kwa nafasi yake anapaswa kumbembeleza na kumheshimu mume wake katika nyanja zote za maisha yao. Waswahili wanasema: **"**Heshima kitu cha bure". Msanii anawataka wanandoa hao kutowadharau waume zao kwa kuwaita majina yasiyostahiki, mume aitwe bwana na sio babu, mume amwite mkewe kwa majina mazuri asiseme "mwanamke wangu " ni matusi makubwa, hii ndiyo heshima katika ndoa.

Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika inaakisi vyema dhima za wimbo huu. Katika hali ya kawaida wanandoa wanahitaji kuheshimiana, mke amheshimu mume na mume amheshimu mke. Kuwepo kwa hali hii katika maisha ya wawili hao ni kujenga misingi imara ya kuifanya ndoa yao idumu.

Aidha, Kiuhalisia mwanamke na mwanamume wanapofikia umri wa utu uzima (baleghe) basi ni wajibu wao kila mmoja kupata mwenziwe wa kumliwaza na kumtuliza nafsi. Kinyume cha hayo ni kwenda kinyume na maadili ya jamii, ndipo pale msanii aliposema "mwari wako amekuwa, kuolewa ni wajibu".

Maelezo haya yanatiliwa mkazo na mtaalamu Seif (2011) wakati alipouelezea unyago kwa jinsia ya kike. Alisema, unyago humuandaa mwanamke (msichana) kukabiliana na utu uzima. Hii ni pamoja na doa, miko ya mila na mafunzo ya maisha kwa jumla. Suala analaolitilia mkazo mtaalamu huyu yamejificha ndani ya mafunzo anayopatiwa msichana wakati akiwa unyagoni ambayo ni pamoja na kumuheshimu mume wake.

**5. MWANANGU**

Nilipokuwa mdogo wee, mwanangu oyaa!!

Mama alinihusia wee, mwanangu oyaa!!

Mtu hubadili nguo wee, mwanangu oyaa!!

Hazibadili tabia wee, mwanangu oyaa!!

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo huu unajaribu kutoa usia kwa binti kuhusiana na maisha katika ndoa.

**DHIMA**

Wimbo unalenga kumfunda binti kutobadili tabia zake mara tu aingiapo katika ndoa. Msanii anasisitiza kwamba mtu hubadili nguo si tabia. Mtafitiwa Bi Bahati Rajab wa Uzini, alifafanua, wari walio wengi mara tu baada ya kuingia katika ndoa hubadili tabia zao kwa kuwafanyia watu jeuri na dharau tabia ambazo hazipendezi kwa waungwana. Wanandoa wanatakiwa wawe na tabia njema kwa watu wa marika na jinsia zote, hali ambayo hujenga mapenzi miongoni mwa wanajamii kwa jumla.

Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika imefungamana sana na uchambuzi wa dhima hii. Maumbile yao wanawake walio wengi ni wenye jeuri, maringo na majivuno baada ya kuingia katika ndoa. Huonekana kubadili tabia na mienendo yao ya asili, jambo ambalo halipendezi kwa jamii ya wanandoa.

Shaaban Robbert na Gibbe (1981) wanaonekana kwenda samabamba na dhima ya wimbo huu, pale waliposema kuwa, nyimbo hutumika katika kuwaelimisha wanandoa kwa lengo la kupata maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, hekima, pamoja na adabu nzuri. Wimbo huu unajaribu kuwaelimisha wanandoa watarajiwa kuwa na adabu nzuri. Tendo la kutobadili tabia walizokuwa nazo wakati walipokuwa chini ya uangalizi wa wazazi wao, linapaswa kuendelea hata wakati wakiwa kwa waume zao.

## 6. KAKAE MWANA NYUMBANI KWAKO

Kakae mwana, kakae

Ukakae na mumeo

Siri ya nyumba ni kunga

Kupata au kukosa

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Siri ya nyumba ni ya mke na mume. Msanii wa nyimbo hii anawakumbusha wanajamii kuhusu siri ya wanandoa ndani ya nyumba zao. Hazisemwi nje ya chumba chao ni siri yao.

**DHIMA**

Dhima kuu ya wimbo huu ni subira kwa wanandoa. Mume ana wajibu wa kumtimizia mke wake haki zake za msingi ikiwemo chakula, mavazi na pahala pa kuishi kwa mujibu wa uwezo wake. Wanandoa watarajiwa wanapatiwa indhari kuwa, mume atakaposhindwa kumpatia chochote ni busara kwa mke kuwa na subira kwani katika maisha, kuna kupata na kukosa. Subira katika maisha ya ndoa hujenga huruma baina ya mke na mume.

Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika inaakisi vyema dhima ya wimbo huu. Katika hali halisi, wanandoa wanapaswa kuvumiliana na kustahamiliana kwa yale yote yatakayotokezea ndani ya ndoa zao, makubwa na madogo, ya siri na ya dhahiri. Wanandoa watakapoyaweza haya wataweza kuzijenga, kuzimarisha na kuzidumiosha ndoa zao.

**7. PWANI**

Huko pwani kuna uwa

Rangi yake ni manjano

Ukitaka kulichuma

Ulichumiye sindano

Kuolewa si besera

Ndoa ni masikizano

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo huu umehusisha mkabala wa ndoa na pwani ambako kunapatikana mauwa yenye rangi ya manjano. Wimbo umetumia lugha ya ishara katika kuwasilisha ujumbe kwa wanandoa watarajiwa Maneno, uwa, pwani na sindano, yote yametumika kiishara. Neno **"**pwani," limetumika likiwa na maana ya maisha ya ndoa kwa jumla. Pwani ina mawanda mapana, ndani yake mna mkusanyiko wa vitu vingi samaki, matumbawe, majini na masubiani. **"**Uwa," likiwa na maana ya matukio yatokezeayo katika ndoa, mazuri na mabaya**.** Sindano lina maana ya mbinu watakazozitumia wanandoa katika kutatua matatizo yatakayowakabili wakiwa katika ndoa zao.

**DHIMA**

Msingi ya wimbo huu ni kuwaweka bayana wanandoa watarajiwa kuhusu maisha yao ya ndoa. Maisha ya ndoa yamefananishwa na bahari (pwani), kutokana na upana wake. Falsafa nzima ya maisha inapatikana katika ndoa. Wanandoa watakumbana na mengi, makubwa na madogo, mazuri na mabaya, ya kupendeza na ya kuchukiza.

Wanandoa watarajiwa wanapatiwa mafunzo ya msingi kuwa, katika ndoa zao watakutana na mengi na ni wajibu wao kupima na kuamua ni mbinu gani mwafaka zitakazoweza kuleta maelewano wakati wa kutokezea matatizo. Ni mbinu gani watumie ili kuleta mustakbali mwema wa maisha baina yao.

Nadharia ya Dhima na Kazi inakwenda sawia na uchambuzi wa dhima hii kwa wanandoa. Wajibu wa wanandoa wakiwa katika ndoa zao ni kuwa na uchaguzi wa nini cha kufanya wakati wa kutokezea matatizo katika ndoa zao. Isiwe kukurupuka na kufanya mambo yasiyo muafaka katika kutoa maamuzi.

Aidha, nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika nayo inajitokeza katika uchambuzi wa dhima hii. Katika hali halisi ya maisha ya wanandoa matatizo, shida, na sintofahamu nyingi zaweza kutokezea baina yao. Cha msingi ni kuchukua hatua za kujenga maelewano baina yao na si vyenginevyo.

Maelezo haya yanatiliwa mkazo na mtaalamu Lucas (1975) alipozungumzia nyimbo za msanja na jando kama ni utamaduni wa mwafrika. Alisema nyimbo hizi hutoa mafunzo, malezi, na maadili mema yanayowasaidia wanajamii kujua namna ya kuishi kulingana na matumizi ya nyimbo hizo. Hali hii inasawiri vyema matumizi ya nyimbo hii kulingana na jamii. Wananajamii wanapaswa kujua kuwa, maisha ya ndoa si starehe tu bali ni maisha yaliyojaa misukusuko, matatizo, migogoro na migongano baina yao. Ni busara kujijengea misingi imara itakayoboresha ndoa zao.

**8. MWANANGU**

Maneno haya ya nani

Yako wewe waambiwa

Ukifika kwa mumeo

Yako wewe waambiwa

Uwapende na wakwezo

Yako wewe waambiwa

Pamoja na shemejizo

Yako wewe waambiwa

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo umeanza kwa kutoa usia kwa wanandoa watarajiwa kuhusu maisha yao ya ndoa. Msanii wa wimbo huu amekuja na maneno mazuri kwa wanadoa hao, ni muongozo mwema kwa maisha yao.

**DHIMA**

Wimbo unalenga kutoa fundisho kwa wanandoa watarajiwa kuwapenda watu na jamaa za waume zao kama vile mama, baba, na ndugu zao. Mtafitiwa Bi Bahati Rajab alisema kuwa, wanawake wengi katika jamii zetu wana tabia ya kuwachukia jamaa na ndugu za waume zao. Wimbo huu unatoa nafasi kwa wanandoa watarajiwa wajirekebishe na suala hili. Wafikapo kwa waume zao hawatakiwi kuwadharau, kuwakebehi, kuwachukia, kuwabaguwa na kuwabeza jamaa za waume zao, bali wajenge nao mapenzi na huruma wakati wote, tabia hiyo itawawezesha kustawisha ndoa kwa pande zote za mke na mume.

Maelezo haya yanatiliwa mkazo na nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika. Katika hali halisi tunawaona baadhi ya wanawake mara tu baada ya kuolewa huwa na tabia ya kuwachukia ndugu na jamaa za waume zao ambao hapo kabla walikuwa na mapenzi

makubwa sana. Hali hii inasababishwa na tabia za kimaumbile walizonazo baadhi ya wanawake za kujijengea dharau, kiburi na uchukivu kwa jamii hiyo.

Mulokozi alipoelezea nyimbo kwamba zinasimulia na kuelezea matukio yanayojitokeza katika jamii zikiwa na malengo ya kufunza, kuelimisha, kukosoa na kuburudisha, aliweza kuyatilia mwega maelezo yaliyoelezea dhima ya nyimbo hii. Wasanii walikuwa mstari wa mbele kuielimisha na kuifunza jamii ya wanandoa kuhusu jinsi watakavyoweza kuishi na wakwe zao, shemegi zao, jirani zao na jamii yote itakayowazunguka.

## 9. NDUGU YANGU

Ndugu yangu nakuasa, ndoani waelekea
Utayakwaa mashaka, na matuta kwenye ndoa
Usikimbilie talaka, Ilahi anachukia
Wazazi kuwakimbilia, ugomvi ukitokezea.

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo umejaribu kuelezea jinsi maisha ya ndoa yalivyo. Ndani yake kuna mambo mengi ambayo yaweza kutokezea migogoro, migongano, raha, karaha, mazuri na mabaya.

**DHIMA**

Dhima kubwa inayojitokeza katika wimbo huu ni kwa wanandoa kuwa na subira na uvumilivu pale yanapotokezea matatizo katika ndoa zao.

Wanandoa wanapewa fundisho hili kwa kupewa indhari juu ya mbinu za kutatua matatizo katika ndoa zao. Msanii anapendekeza njia ya kuwaona wazazi wa pande zote, upande wa mke na wa mume katika kusuluhisha migogoro yao na sio talaka. Mtafitiwa Bi Maryam Ali wa Mitakawani aliinasibisha dhima ya wimbo na mafundisho ya Bwana Mtume Muhammad (SAW) kwamba, “talaqa ni halali lakini ameichukia Mwenyezi Mungu”, hivyo, si busara kwa wanandoa kuchukua uwamuzi wa kupeana talaka kabla ya kupata ushauri kutoka kwa wazazi.

Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika inakwenda sambamba na uchambuzi wa dhima hii. Ndani ya jamii ya wanandoa hakuachi kujitokeza matatizo, migongano, migogoro ya hapa na pale baina ya wanandoa. Cha kufanya ni kuwashirikisha wazazi wa pande zote mbili, upande wa mke na wa mume katika kutoa suluhishi la matatizo yao, hii yaweza kuboresha ndoa na kuwafaya wanandoa kuishi kwa muda mrefu. Katika hali ya maelewano na mashirikiano katika nyanja zote.

**10. SHOGA**

Shoga wengine si shoga

Watakuibiya!!

Utawaona hawatoki kwako

Kuja kutembea!!

Na wakimuona mume wako

Macho wakodoa!!

Tahadhari Sana haooo

Watakuja kukuibiya!!

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Shoga ni rafiki wa kike wa mwanamke. (Kamusi ya Kiswahili Sanifu: 2004). Shoga aliyetajwa katika wimbo huu ana tabia zisizopendeza kwa wanandoa, mara nyingi anapowatembelea wanandoa, hujipendekeza kwa mume wakiwa na lengo la kumpora mume wa nyumba hiyo. Anaweza kuiharibu ndoa ikiwa mume ni dhaifu asiyejijuwa na asiyejiweza.

**DHIMA**

Msanii analenga kuwafunda wanandoa watarajiwa juu ya athari hasi za mashoga kwenye ndoa za watu. Athari kubwa iliyotajwa ni kuvunjika kwa ndoa. Kwa mujibu wa mtafitiwa Bi Mwanahawa Makame Mzee wa Mitakawani, shoga huonyesha tabia ya ukarimu na ukaribu mkubwa. Mume ni kiumbe dhaifu. Inamwia rahisi kutoka katika ndoa yake na kujihusisha na mapenzi na shoga wa mke wake.

Maelezo ya dhima ya wimbo huu, yanatiliwa kani na nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika. Katika hali halisi ya jamii za wanandoa huwa na mahusiano ya karibu na watu wa nje ya familia zao (mashoga). Watu hawa kwa kweli ni hatari sana kwa ndoa za watu. Mara nyingi ndio wanaoziharibu ndoa kwa kujihusisha na mapenzi na waume za watu. Wakati mwengine shoga hawa hufanya mambo yanayoashiria mapenzi na mume wa watu kwa siri kubwa bila ya mke husika kutambua kinachoendelea, hatimae ni kuvunjika kwa ndoa.

Msokile anasema kwamba dhamira za nyimbo ni lazima zilingane na hadithi kwa maana ya kwamba ujumbe unaopatikana ni lazima ulingane na jamii yenyewe. Hali hii inasawiri vyema dhima ya wimbo huu kwa sababu wimbo unatoa mwangaza kwa

wanandoa watarajiwa watakapofika katka ndoa zao, wawe na tahadhari kubwa sana na mashoga kwani hawana mwisho mwema kwa ndoa zao.

**11. SORORE MWANA**

Sorore mwana, sorore mwana

Usiwe na jicho la naje

Mwana, somo akutowe nnje.

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wimbo unatoa fundisho la kudumu kwa wanadoa watarajiwa kujiepusha na zinaa.

**DHIMA**

Somo anamhadharisha mwari wake juu ya kuepukana na suala la zinaa katika ndoa. Msanii Bi Talhiya Masoud alisema kuwa baadhi ya wanandoa hushindwa kustahamili na kuridhika na waume walio nao na badala yake hujaribu kuzisaliti ndoa zao kwa kujihusisha na mapenzi na wanaume wa nje. Hivyo wimbo unalenga kumtuliza mwanamke, atulie ndani ya ndoa yake na kuridhika na mume aliyekuwa naye. Mazoea hujenga tabia.

Msingi wa nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika unakwenda sambamba na maelezo ya dhima ya wimbo huu. Katika hali halisi ya maisha ya wanandoa, kitendo cha zinaa hakipendezi na hakikubaliki kabisa baina ya wanandoa. Hata kitabu kitukufu cha Qur-an kinatoa mafundisho hayo kwa kusema: "Na wala msiikaribie zinaa, hakika ya zinaa ni uchafu ulio wazi na na njia ya upotevu". Hivyo wasanii wa nyimbo za singo, wanandoa, makungwi na masomo walipotoa taaluma hii kwa wanandoa watarajiwa walikuwa wanakwenda sambamba na wakati katika kuielimisha jamii.

Mtaalamu Gibbe (1980) hakua nyuma kulizungumzia suala hili la kuwa na maadili mema kwa jamii ya wanandoa watarajiwa. Alisema, nyimbo hutumika katika kuwaelimisha wanandoa kupata maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, hekima pamoja na adabu nzuri. Haya yote yameelezwa kupitia wimbo huu, jamii ikiweza kujizuia na kitendo cha zinaa basi itaweza kuwa na maadili mema, hekima, busara, ustahamilivu pamoja na kuwa na adabu nzuri.

**12. MTI**

Mti huu, mti huu
Wa ajabu, mti huu,
Naupanda na jua, na kasikaazi mkuu
Kwa jamii nauliza manyakanga
Waitwaje mti huu?

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Wasanii wametumia neno “mti” likiwa na maana ya “uume” “Kupandwa” hapa, imetumika kama ni msamiati maalumu ambao unahusisha tendo la ndoa. Taswira hii inaendana na sifa za uume ambao kimsingi huhitaji kuimarishwa katika kipindi chote cha maisha ya wanandoa. Uume hauna subira usiposhibishwa kisawasawa una ila ya kubabaika.

**DHIMA**

Dhima kubwa inayozungumzwa katika wimbo huu ni mke kumtimizia mume haki yake ya msingi katika ndoa. Mtafitiwa Bi Mafunda Saleh Ali alisema, ndoa hutimia na humea kwa kuwapo kwa kumtimizia mume haki yake ya msingi. Mke anapaswa

kumtekelezea mume wake haki hiyo ya msingi kwa nyakati zote. Mume ni kiumbe dhaifu ambaye anashindwa kustahamili pindi mke akimkatalia suala hilo. Ni wajibu wa wanawake kuwaridhisha waume zao katika kuwatekekelezea haki hiyo ya msingi katika ndoa. Muumba Aliweka suala hilo kuwa ni kitulizi cha nafsi cha wanandoa.

Nadahria ya Uhalisia wa Kiafrika inaonekana kwenda sambamba na uchambuzi wa dhima ya wimbo huu, kwa vile tu inaelezea matukio katika uhalisia wake. Katika mazingira ya kawaida ya wanandoa , mke ni wajibu wake kumtimizia mume haki yake ya msingi katika ndoa , wakati wowote, pahala popote, ikiwa hakuna sababu za udhuru wa kisheria.

Sengo (1991) kwa upande wake naye anayasahadidia maelezo haya pale alipoelezea kuhusu mila na tamaduni za watu wa pwani.Alisema kuwa wasichana huko unyagoni walitakiwa kuyajua mambo ya kiutu uzima, ndoa na namna ya kuyamudu maisha.Hali hii inarejelea moja kwa moja dhima ya wimbo huu kwani kitendo cha mke kutimiza haki ya ndoa kwa mume wake ni kitendo cha kuyaelewa maisha ya kiutu uzima.

**13. JAMBO SI JAMBO**

Na jambo si jambo

Usende sema kwa mama

Kuna badiria

Mzazi hufa kwa mwana.

**MAELEZO KUHUSU WIMBO**

Maisha yana mambo mengi. Mengi ya hayo ndizo siri za ndoa. Mengi hayatakiwi kusemwa wanandoa hawana budi kutunza siri za ndoa zao.

**DHIMA**

Dhima kubwa ya wimbo huu ni subira kwa wanandoa. Msanii anawafunda wanandoa watarajiwa juu ya suala zima la kuwa na subira kwa yale yote yatakayojitokeza katika ndoa zao kwa lengo la kudumisha, kuimarisha, na kustawisha ndoa. Kimsinngi wanandoa hao wanapaswa kuwa wastahamilivu kwa yale yote yatakayowasibu wasiwe watu wa kuropoka hovyo kila linalotendeka nyumbani mwao. Mke asiwe mwenye kutoa nnje mambo yanayotendeka nyumbani mwake. Kufanya hivyo ni kujenga migogoro katika ndoa baina yake na mume wake pamoja na wazee kwa jumla. Hayo hufanywa na wasungo wasiofundwa na masomo wao.

Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika inachukua nafasi ya kuyakubali mawazo ya dhima ya wimbo huu, ukizingatia msingi wake wa uhalisia. Suala la kuwa na subira kwa wanandoa ni suala nyeti na muhimu sana katika kujenga ndoa zao. Katika mazingira ya kawaida, wanandoa hawaachi kugongana, kukwaruzana, kuhitilafiana katika masuala tofauti ndani ya maisha yao. Cha kufanya hapa kwa wanandoa ni kuvumiliana na kujenga nyoyo zenye kusubiriana. Kila mmoja anapaswa kuwa mstahamilivu kwa mwenziwe.

Mawazo ya Mulokozi (2013) yanaakisi vyema dhima ya wimbo huu kwa wanandoa kuwa na subira. Mulokozi anasema kuwa nyimbo zote husimulia na kuelezea matukio yanayojitokeza katika jamii zikiwa na malengo ya kufunza, kuelimisha, kukosoa, na kuburudisha. Wimbo huu umelenga kuwapatia mafunzo wanandoa watarajiwa juu ya suala zima la kuwa na subira ndani ya ndoa zao. Ni taaluma muhimu kwa wanandoa hao itakayowapelekea kuishi maisha ya raha ndani ya ndoa zao.

# SURA YA TANO

# HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Kubwa ni kufahamu dhima za nyimbo za singo kwa jamii ya wanandoa. Katika hitimishi ni kutoa majumuishi ya utafiti huu na katika mapendekezo ni kuangalia kitu gani kinachotakiwa kuboreshwa zaidi katika kuendeleza mila na utamaduni kwa lengo la kujenga maadili kwa wanandoa.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ya utafiti huu imeeleza juu ya vipengele vya utangulizi usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahsusi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake. Sura ya pili ya tasnifu hii inahusu utalii wa kazi tangulizi ambazo moja kwa moja zinahusiana na mada ya utafiti.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imewasilisha mbinu za kukusanyia na kuchambulia data, muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, uteuzi wa watafitiwa. Vipengele vingine ni aina ya data zilizokusanywa, data za msingi na data za upili, mbinu za kukusanyia data ambazo ni mbinu za usaili, hojaji na ushuhudiaji. Aidhani, mtafiti ametumia mbinu ya kimaelezo katika uchambuzi wa data. Baada ya hapo vimeelezwa vipengele vya usahili na maadii ya utafiti.

Sura ya nne imewasilisha uchambuzi wa data za utafiti. Uwasilishaji huo ulifanywa kwa kuzingatia madhumuni mahasusi ya utafiti huu. Kwa kuzingatia hilo, nyimbo

zinazoimbwa katika sherehe ya singo, pamoja na dhima zake kwa jamii, vimewasilishwa. Sura ya tano ndiyo inayotoa muhtasari, hitimishi, matokeo na mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.3 Hitimishi

Utafiti huu umefanikiwa kukamilisha madhumuni yake mahsusi ambayo yalikuwa ni mawili. Madhumuni mahsusi la kwanza yalilenga kubainisha nyimbo zilizoimbwa katika sherehe za singo. Madhumuni ya pili yalilenga kuchambua dhima za nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo.

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kwamba jamii ya watu wa Uzini bado inaendeleza mema ya utamaduni wake wa kuwasinga wanawari kwa kutumia nyimbo ambazo ndani yake zimesheheni mafunzo toshelevu kwa maisha ya wanandoa.

Watafitiwa wote waliohojiwa katika utafiti huu wamethibitisha umuhimu wa kuwepo na kuendelezwa kwa utamaduni huo kwa sababu nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za singo zimeonekana kuwa na nafasi kubwa na nzito kwa jamii zetu, nafasi ambazo hulenga kuwapatia mafunzo wanawari ambao wanaandaliwa kuyakabili maisha halisi ambayo ndiyo maisha yao ya ndoa katika nyanja tafauti za kimaisha, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kimaendeleo.

Kimsingi nyimbo za singo zinalenga kuwapatia wanawari mafundisho yafuatayo;

(a) Kuheshimiana katika maisha ya ndoa.

(b) Kuwatimizia waume haki zao.

(c) Kuwatii waume zao.

(d) Kuwa na tabia na mwenendo mzuri kwa waume zao.

(e) Kujenga moyo wa subira katika kukabiliana na matatizo ya ndoa zao.

(f) Kuishi vizuri na majirani zao.

(g) Kuepuka uhusiano wa kimapenzi na shemeji zao

(h) Kuwatii, kuwaheshimu, kuwahurumia, na kuwapenda wakwe zao.

(i) Kuepuka kuwaroga waume zao.

(j) Kuwaandalia chakula kizuri waume zao.

(k) Kujenga tabia nzuri zenye kuvutia kwa jamii ya waume zao.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulihusisha nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya singo pamoja na dhima kwa binti ambaye anatarajiwa kuingia katika maisha yake ya ndoa. Tunapengekeza utafiti mwingine ufanyike kuhusu nyimbo za singo kwa vijana wa jinsia ya kiume ambapo wataweza kujipatia mafunzo yaliyo mema kwa lengo la kuzijenga ndoa zao. Tunapendekeza utafiti mwengine ufanyike uangalie ubora na udhaifu wa nyimbo za singo kwa mabinti waliofanyiwa singo na kuangalia kwa kiasi gani wamefanikiwa katika kuzijenga ndoa zao.

**MAREJELEO**

Adam, O. A. (2006). *Matumizi ya Kiswahili katika Nyimbo za Kizazi Kipya*. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar: Zanzibar

Ali, H. S. (2005). *Mafumbo Yanayopatikana katika Nyimbo za Harusi katika Ndowa za* Unguja. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar: Zanzibar.

Aranson, J. (1992). *A Pragmatic View of Thematic Analyisis in the qualitative Research Methods in Nursing* Oroland F.L Grum and Stratton.

Babbie, E. (1999). The *Basics of Social Research.*. Belmont: Wardsworlth Publishing Company.

BAKIZA, (2010). Kamusi *la Kiswahili Fasihi*. Nairobi: Oxford University Press.

Balysidya, N. L. (1987*). "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi"* Mulika namba 19, Dar es Salaaam: TUKI.

Beyanga, A. (2004). *"Taswira ya Ngombe katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Washubi"* Tasnifu ya Uzamili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Cohen, L. M. and Keith, M. (2000). *Research Methods in Education (5th edition)* London: Routledge Publishers

Masebo, J. A. and Nyangwine, N. (2006). *Kiswahili Kidato cha 3 na 4*. Dar es Salaam: The Oral Literature in Africa General Bookseller Ltd.

Mollen, L. M. (2008). Utafiti wa Lugha za Asili Tanzania. Semina ya Utafiti kwa maafisa wa Utamaduni. Dodoma, Tanzania.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Khatib, M. S. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mrikana, S. E. (2010). *"Kejeli na Fasihi ya Kiswahili Tanzania, katika Swahili Forum,* Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mzee, A. F. (2011*). Athari za nyimbo za taarab ya mipasho kwa jamii ya Wazanzibar.* Dodoma: Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Msokile, M. (1981a). Nafasi *ya Nyimbo za Fasihi simulizi katika Jamii Iliyomdikwa*. Makala za Fasihi simulizi Chuo Kikuu Cha Dar-es –Salam.

Mulokozi, M. M. (1996b). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (B.A.ED) PHD. Dar eS Salaam, Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Muhammed, O. S. (2010). Mchango wa Nyimbo za Unyango katika Kumkomaza Mwari Kinyumba. Ripoti Mintarafu Wilaya ya Kinondoni nchini Tanzania. Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda.. Kampala, Uganda.

Muhando, P. na Balysidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia Na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. M. V. (1993). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: Kitabu Commercial Printing Company Ltd

Nkwera, F. M. V. (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Shaaban, R. na Gibbe, A. G. (1980). *Mitaala ya Lugha na Fasihi Tanzania*. Dar-es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sengo, T. S. Y. (1972). Hadithi za Kikwere: Kioo cha Lugha namba 2. Dar es Salaam: Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (1973*). Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii.* Jarida la Kiswahili. Dar-es Salaam: TUKI.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*, Dar es Salaam: AKADEMIA.

Sengo, T. S. Y. (1987). *Fasihi Simulizi, Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Nyanza Publication Agency.

Sengo, T. S. Y. na Kiango, S. D. (1973). *Hisi zetu.* Dar-es-Salam: Tanzania Publishing House.

Shaaban, R. (2004). *Kielelezo cha Fasihi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishing Company.

Senkoro, F. E. M..K . (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TAKILUKI, (1983). Fasihi *Simulizi ya Zanzibar*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing house.

Wamtila, K. W. (2002). Kamusi *ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Kenya Oxford University Press.

Wamtila, K. W, (2003*). Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Chuo Kikuu Dar-es-Salam. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Wamtila, K.W. (2008). *Kanzi za Fasihi Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vde- Muwa Publishers Limited.

# VIAMBATANISHI

## Kiambatanishi 1: Hojaji La Utafiti Kwa Watafitiwa

**MADA: Kuchunguza Dima za Nyimbo za Singo**

Msimamizi / Mtafiti …………………….. Tarehe ………………

Maelekezo:

Kwa moyo wa upendo na huruma unaombwa kutoa ushirikiano kwa kadri uwezavyo katika kufanikisha mchakato wa utafiti huu. Dodoso hili limeandaliwa kwa lengo la utafiti huu na si vyenginevyo. Hivyo, kuwa huru katika kulijaza. Soma maswali yote kwa uangalifu na makini kisha jibu maswali kadri ujuavyo kwa kuweka alama (√) au maneno muafaka katika sehemu husika.

TAARIFA ZA MTAFITIWA.

1 Jina (sio lazima) ……………………………………….

2 Jinsia (i) kike [ ] ( ii) Kiume [ ]

Sehemu unayoishi ……………………………………

Mkoa ……………………………..

Wilaya ……………………………….

Shehia ………………………………….

Tarehe …………………………………

Je, umewahi kuhudhuria katika sherehe ya singo?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

Kama ndio ni nyimbo zipi zinazoimbwa katika sherehe ya singo?

Taja nyimbo zisizopungua tano

(a) ………………………………………………………………………

(b) …………………………………………………………………………….

( c) ……………………………………………………………………………

(d) …………………………………………………………………………….

(e) ……………………………………………………………………………..

3 Watumiaji wakuu wa nyimbo za singo ni akina nani?

(i) Wazee [ ] (ii) Watoto [ ] (iii) Makungwi [ ] (iv) Walimu (v) Vijana [ ]

4 (a) Jee kuna vipera vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika nyimbo za singo?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

(b) Kama ndio, taja vipera hivyo

(i) ……………………………………..

(ii) ……………………………………….

(iii) ……………………………………………

(iv) …………………………………………….

5 Taja dhima za vipera hivyo kwa wanandoa watarajiwa.

(i) ………………………………. (ii) ……………………………………

(ii) ……………………………… (iii) …………………………………….

(iv) ……………………………… (v) …………………………………….

6 (a) Jee! nyimbo za singo zina mchango wowote kwa jamii ya wanandoa watarajiwa?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

(b) Kama ndio, taja mchango unaopatikana

i) …………………………………………..

ii) ……………………………………………

iii) ……………………………………………….

(c) Kama hapana toa sababu zako

(i)………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(ii)………………………………………………………………………………………

…………..……………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………

(iii) ……………………………………………………………………………….

7 Elezea mtazamo wa wazee juu ya nyimbo za singo.

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………

8 Jee! kuna umuhimu wowote wa kuendelea kuwepo kwa sherehe hii ya singo?

(i) Ndio [ ] (ii) Hapana [ ]

Kama ndio, taja sababu tano za msingi

(a) ……………………………………………………………………………….

(b) ………………………………………………………………………………..

(c) …………………………………………………………………………………….

(d) …………………………………………………………………………………….

(e) ………………………………………………………………………….……..

Kama hapana, toa sababu tano za msingi

(a) ……………………………..……..……………..…………………..

(b) …………………….……………..………………..……………………..

(c) ……………………….……………………..…..……………………

(d) ……………………………………….…………………………...

(e) ……………………………………………………………………..

9 Unafikiri ni kwa nini nyimbo za singo zimeanza kupoteza uhalisia wake?

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

……………………………………………………

10 Toa maoni yako kuhusu nyimbo za singo.

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

**Kiambatanishi 2: Nyimbo Zinazoimbwa Katika Sherehe za Singo**

1 .MUME

Ukitaka mume akae, kutandika kuna maanae,

Ukitaka mume aishi, kutandika kuna maandishi,

Ukitaka mume adumu, kutandika kuna maalumu.

(Bi Maryam Moh'd Ali. Mitakawani)

2 . SHELA

Shela na sheule mwanangu funika upatu

Na wendako mwanangu ni mbele ya watu

Usihusudike na macho ya watu

Iyooo ada ya harusi yoyoyo furaha yao salama

(Bibi Mgeni Ali Moh'd, Uzini Mshomarini)

3. KUNGWI

Kungwi mwambie mwario

Asiwache ufunguooo

Akiwacha ufunguo

Watafunguwa wenziwe,

Na kama hakufyagia

Watafyagia wenziwe,

Na kama hakufukiza

Watafukiza waenziwe.

(Bibi Bahati Hassan: Uzini Kibombani)

4. MSUMARI WA KIZUNGU

Msumari wa kizungu, haulali yeka

Hata bafuni, haulali yeka

Hata sebuleni, haulali yeka

Hata jikoni, haulali yeka.

(Mgeni Ali Moh'd, Uzini Mshomarini).

5. KAKAE MWANA NYUMBANI KWAKO

Kakae mwana kakae

Ukakae na mumeo

Siri ya nyumba ni kunga

Kupata au kukosa

(Bibi Tatu Ame Suleiman, Mpapa)

6. KERO

Ubeti wakwanza.

Kero keero weee!!! Kero Kerooo

Kero Kerooo wee, Mwanangu Keroooo

Kero kero si jema, lavunja nyumba.

Ubeti wa pili

Akiingia keeero wee, akitoka kerooo

Akikaa keero wee, akisimama kerooo

Kero kero si jema lavunja nyumba.

Ubeti wa tatu

Kangamaare wee, Kangamaree

Ukaangamaare, wee ukangamareee

Unakwenda mijini kwa watu ukaangamaree

Ubeti wa nne

Ukafiche kuche wee, ukafiche kuche

Ukafiche kuche wee, ukafiche kuche

Unakwenda mjini kwa watu ukafiche kuche.

Ubeti wa tano

Unamie chini wee, Unamie chini

Unamie chini wee, Unamie chini

Unakwenda mijini kwa watu unamie chini.

Ubeti wa sita

Ukaone haya wee, Ukaone haya

Ukaone haya wee, Ukaone haya

Kuchungulia mvungu wa mkweo ukaone haya.

KIITIKIO

Kero keeero weee mwanangu kero

Kero kero si jema lavunja nyumba.

(Bibi Khadija Khamis Zahoro, Mgenihaji)

7. ILA

Ubeti wa kwanza

Kila siku majiani, ila hiyoo dada

Leo kwa dada fulani, ila hiyo dada

Na kule takwenda lini, ila hiyo dada

Hilo litakuchongea, ila hiyo dada.

Ubeti wa pili

Na ovyoovyo kununa, ila hiyo dada

Bila sababu ya maana, ila hiyo dada

Mume hajakutukana, ila hiyo dada

Wala hajakusakama, ila hiyo dada

Ubeti wa tatu

Mtu asije kuzonga, ila hiyo dada

Kutaka kwenda uganga, ila hiyo dada

Mume harogwi kwa konga, ila hiyo dada

Hurogewa kwa ukunga, ila hiyo dada

Ubeti wa nne

Ukikogea kitanda, ila hiyo dada

Hilo mume hatopenda, ila hiyo dada

Ukikogea kuranda, ila hiyo dada

Na mapambo kupambia, ila hiyo dada

(Bibi Aviwa Idd Mwadini, Tunduni)

8. MWANANGU

Nilipokuwa mdogo wee, mwanangu oyaa

Mama alinihusia wee, mwanangu oyaa

Mtu hubadili nguo, wee mwanangu oyaa

Hazibadili tabia, wee mwanangu oyaa.

(Bibi Asha Ramadhani, Mpapa).

9. PWANI

Huko pwani kuna uwa

Rangi yake ni manjano

Ukitaka kulichuma

Ulichunie sindano

Kuolewa si besera

Ndoa ni masikizano.

10. ILA

Ubeti wa kwanza

Kuna ila moja ilaaaa

Yako dada ilaaaa

Uchafu uuwache ilaaaa!

Ubeti wa pili

Kuna ila moja ilaaaa

Yako mama ilaa

Kuwapuuza wakwe ilaaaa

Ubeti wa tatu

Kuna ila moja ilaaaa

Yako mama ilaa

Kila siku kwamama ilaaaa

Ubeti wa nne

Kuna ila moja ilaaaa

Yako mama ilaaa

Kusimbulia chakula ilaaaa!!

Ubeti wa tano

Kuna ila moja ilaa

Yako mama ilaaa

Siwezi kupika ilaaaa!!

Ubeti wa sita

Kuna ila moja ilaa

Yako mama ilaaaa

Nyumbani kutofyagia ilaaaa!!

Ubeti wa saba

Kuna ila moja ilaa

Yako mama ilaaa

Ujuba uuwache ilaaa!!!

11. KISIKI

Ubeti wa kwanza

Kisiki sikia mumeo oo!!

Kisiki weee sikia mumeooo!

Jambo la kuambiwa halatuwi moyo

Kisiki wee sikia mumeoooo!

Ubeti wa pili

Kibonongwa ndiye mumeoo

Kibonongwa weeee ndiye mumeooo

Jani la mkungu uzuri wa bure

Jani la mkungu uzuri wa bure

Hili yungiyungi liletwana mayi

Kang'ae ndo mwenye uziwa.

Ubeti wa tatu

Hasa kwani nini tumwa tambuu napopoze!!

Na popozeeeeeeee!!!

Na tambuu njema zenye kileoooo!!!

Zenye kileoooo!!!

Ubeti wa nne

Na tambuu njema zenye kileo

Raha ya mume, kula na nguo

Na maneno mema, yenye kituo

Yenye kituooo!!!

Ubeti wa tano

Hasa kwani, mwenda kualikwa huko Mogadishu hata Amerika

Hata Amerikaaaaa!!!

Ni mbegu njema isiyo na shaka aaaa

Na mwenye kupanda hutumaini

Ni mbegu njemaaaaa isiyo na shakaaaaa

Mwenye kupanda hutumaini

Ubeti wa sita

Atowaye watu muhadharani

Uwe mke stiri mwenye mahaba

Mwenye mwanya kati wenye haiba.

Ubeti wa saba

Sasa kwani kutii mume kuanza asili

Wanazuoni walifasili

Kaanza Mayasa biti Jabiri

Yaya wa Fatuma biti Rasuli

12. MAMA HARUSI

Ubeti wa kwanza

Mama harusi yu wapi?

Aniazime kitabu

Wala usione haya

Hili jambo la thawabu

Ubeti wa pili

Sote tumeyakutia

Kaanza bibi na babu

Mume ukamwite bwana

Usende kumwita babu

Mume ukampe raha

Usende kumpa tabu.

(Salha Soud Mohammed: Mpapa)

13. SHOGA

Shoga wengine wabaya

    Watakuibiya

Utawaona hawatoki kwako

    Kuja kutembeya

Na wakimuona mume wako

    Macho wakodowaaaaa

Tahadhari sana haoooo

    Watakuja kukuibiya.

(Mwanahawa MakameMzee,Mitakawani)

14. UZI NA SINDANO

Nipenyepenyee, kama uzi na sindano

Kama uzi na sindano weee!!!

Nende hamrore somo, pamlango

Penu pariranta ntata x2

(Mafunda saleheAli, Mwalimu skuli ya sekondari Uzini)

15. MTI

Mti huu, mti huu

Wa ajabu mti huu!!

Naupanda na jua na kasikazi mkuu!!!

Mti unakua kua, unapwana

Kwa jamii nauliza manyakanga

Waitwaje mti huu?

(Mafunda Saleh Ali, Mwalimu skuli ya sekondari Uzini)

16. UJIMA

Nataka ujima mwaka huno

Nataka ujima   x2

Na ujima utakao, si wa watoto

Ni watu wazima

Munaliona wapi guludoza kukata mlima?

(Mafunda Saleh Ali, Skuli ya sekondari Uzini)

17. SORORE  MWANA

Sorere mwana x 2

Usiwe jicho lannje

Mwana, somo akutoe nnje.

(TalhiyaMasoud, Mwalimu skuli ya sekondari Mpapa)

18. NJOO NAE


Njoo nae ee njoo naeee!!

Hakuna mwana asiye na mama

Njoo naeeee!!

(Salha SoudMohammed, Mpapa)

**Kiambatanishi 3: Ramani ya Kisiwa cha Unguja Ikionesha Maeneo ya Utafiti**




**Chanzo: Afisi ya Makumbusho ya Zanzibar**